

MAMBO YATAKAYOKUWAPO

 Kwa Ndugu Boone na kusanyiko, haya bila shaka ni majaliwa ma—makubwa kwangu kurudi San Bernardino tena. Mahali hapa panashikilia kumbukumbu nyingi kubwa za siku zilizopita. Na mimi kusikia jambo hilo, ziara ya kuja hapa, na bado ina ushawishi ambao ungali hai, mbona, kwa kweli mtu linakufanya ujisikie furaha kwamba Bwana alituelekeza kuja huku, miaka kadha iliyopita.

² Nilikuwa nimeketi tu pale kwenye mahali pa kuegeshea magari, sasa hivi tu, nikijaribu kukumbuka moja ya matukio yaliyotukia. Kulikuwa na Bibi Isaacson aliyekuwa mkalimani wangu huko Finland, kwenye uamsho wa Kifini, naye alikuja kwenye gari nilipokuwa tu nikiondoka. Naye akasema, “Sauti Yako ya Finland.” Nami sijui kama Bibi Isaacson anaisha mahali hapa. Sikujua. Asingeweza kuwapo usiku wa leo, je! ndivyo? Bibi May Isaacson, naye anatoka Finland.

³ Halafu jambo jingine kubwa lililokuja kwenye kumbukumbu zangu, lilikuwa ni maskini mhudumu mwanamke kwenye mkahawa ambapo mimi hula, mahali fulani karibu, wanapaita Antlers Hotel. Ninaamini hilo ni kweli, sasa. Na maskini bibi huyo alikuwa na... Nilikuwa nikiomba pamoja naye. Alikuwa... Yeye, msichana mzuri, bali hakuwa Mkristo. Nilimwalika kwenye mkutano. Naye alikuwa amempoteza mtoto wake mchanga, na ninaamini ya kwamba mumewe, walikuwa wametengana. Nasi tulikuwa tukiomba ya kwamba wangepatana na mume wake, ama wangepatana, pamoja. Kwa hiyo, hata sijui kama maskini bibi huyo mdogo angeweza kuwa yupo hapa. Unaona? Ninii...

⁴ Na halafu tukio lingine lililotukia, lilikuwa ni la mtoto mchanga aliyeletwa kutoka mahali fulani, umbali wa mwendo wa gari wa siku moja hivi. Naye alikuwa amekufa, na alikuwa amelazwa mikononi mwa mamaye. Naye akafulufuliwa. Je! huyo... Je! mtu huyo angekuwa yupo hapa? Na katoto hako kalikuja, ninaamini, kutoka kwenye mkoa wa huku, karibu na hapa, lilikuwa ni juu ya hapa. Naye maskini mama huyo alikuwa anaendesha gari usiku kucha, na baba, na maskini mama huyo ameketi pale, kwa huzuni, ameshika maskini maiti ya mtoto wake mchanga aliyekuifa. Ndipo nikawazia, “Imani kama hiyo!” Kama ningalikuwa mnafiki aliye mkubwa sana duniani, Mungu angaliiheshimu imani ya mama huyo.

Nikimshika mtoto huyo mchanga mikononi mwangu, namna *hiyo*, huku nikiomba. Akapata joto, akaanza kusogea, akafungua macho yake madogo. Nikamrudishia mama yake. Kwa hiyo, walikuwa wametokea mahali fulani. Sidhani

walikuwa Wapentekoste, hata hivyo. Walikuwa ninii tu... Ninaamini ilikuwa tu ni kanisa fulani, ambalo kutoka... Hata sijui kama walikuwa Wakristo, ama la. Sikuwaliza kamwe. Nilikuwa nimefurahia sana juu ya mtoto huyo mchanga kufufuliwa tena.

Tangu wakati huo, Ndugu Boone, mambo mengi yametokea. Bali tungali tunamtumikia Mungu ye ye yule Ambaye anadumu kuwa ye ye jana, leo, na hata milele.

5 Nikiangalia tu kila mahali, ninamwona Ndugu Leroy Kopp akiketi hapa. Ni mara ya kwanza nimemwona kwa muda mrefu. [Ndugu fulani anasema, "Anaitwa Paulo Kopp hapa."—Mh.] Paulo. Ni kweli. Leroy ni baba yako. Ni sawa. ["Naye—naye yuko Urusi, usiku wa leo, kwa hiyo mwombeeni."] Loo, jamani! Urusi. Vema, hivyo ni, ninajua, askari huyu hodari kule, yuko kule katika shughuli za Mfalme. ["Sawa."] Kwa hiyo, kwa kweli nina furaha kuwapo hapa na kumsikia mhudumu huyu kijana akisema alivuvuviwa na huduma tuliyokuwa nayo wakati tulipokuwa hapa. Hilo linafurahisha jinsi gani!

Nami ninatumaini sasa, ya kwamba, nikijua twapaswa... Watu wamesimama, wala hatutakaa sana. Tunazikumbuka zile ibada kuu za uponyaji.

6 Halafu, ninasikia ya kwamba kuna ndu—ndu—ndugu hapa jirani, mahali fulani, anayeendesha uamsho wa uponyaji, Ndugu fulani aitwaye Leroy Jenkins. Ninaamini hilo ni kweli. Na kwa hiyo ninashukuru sana, nikitumaini ya kwamba Bwana anambariki na kumpa ibada kubwa, kubwa mno. Ni-...

Jamani, niljisikia nimeheshimiwa sana, usiku wa leo, kuja kwenye kanisa kama hili. Daima hujisikia vizuri zaidi katika jengo la kanisa kuliko ninavyojisikia katika vyumba hivyo vya mikutano. Hakuna kitu dhidi ya chumba cha mkutano. Lakini, unajua, mimi... Huenda ikawa ni ushirikina, ama na ninii tu... Inaonekana kwangu kama ni kweli. Unaona? Wao... Unaingia kwenye kumbi hizo za mikutano ambako kuna mapigano ya ndondi, kupigana miereka, tamthiliya ya vichekesho, kila kitu kingine kikiendelea, inaonekana roho wachafu wanabakia mahali hapo. Sasa, huo huenda ukawa ni ushirikina, lakini huo sio hivyo. Bali wakati unapoingia kanisani, wewe... kwa kawaida, bila shaka kusanyiko la kiroho, inaonekana kana kwamba, hiyo ni kusema, u—unajisikia huru zaidi, kama kwamba kuna—kuna jambo fulani. Uwepo wa Mungu upo. Unajua, panaonekana ni pa tofauti. Sijui jengo linaumba mazingira gani, bila ni mahali watu wanapokusanyika. Bila shaka, watu, wale wale, ndio wanaokusanyika mahali pengine, bila wako kwenye hayo maeneo maovu. Labda ni mimi tu ninayefikiria namna hiyo. Lakini, hata hivyo, nina furaha kuwa hapa usiku wa leo.

⁷ Na sasa hatutaki kuwaweka kwa muda mrefu sana, kwa sababu ya wasikilizaji ambao wanasmama. Nasi tunaenda, kesho usiku, mahali fulani pengine hapa. Hata sijui ni wapi. Ni karibu na hapa. [Ndugu fulani anasema, “Jumba la Mikutano la Orange Show.”—Mh.] Ati wapi? [“Jumba la Mikutano la Orange Show.”] Jumba la Mikutano la Orange Show, kwa ajili ya ibada za kesho usiku. Mimi... Hii iko kati ya ninii, ninazungumza kwenye ziara ya wa—wafanyabiashara wa kundi la Wafanyabiashara wa Full Gospel. Ambalo, nilikuwa na majaliwa ya kuzungumza kote ulimwenguni, kwa ajili yao. Na kwa hiyo kati yao, rafiki mpendwa sana alitualika hapa, nasi tuna furaha kuwa katika kusanyiko hilo usiku wa leo.

⁸ Sasa, kabla hatujafungua Biblia... Sasa, mtu ye yeyote aliye na nguvu za kimwili anaweza kuifungua namna *hii*. Unaona? Lakini inamhitaji Roho Mtakatifu kutufungulia Neno, kufungua ufahamu wetu na kuyafunua Maandiko. Ninaamini Biblia. Ninaamini kwamba Hilo ni Neno la Mungu. Ninaamini ya kwamba dunia, ama watu wa duniani, watahukumiwa siku moja kwa Neno hili. Sasa, hilo linaweza kuonekana la kushangaza. Sasa, kuna wengi wanaotofautiana na wazo hilo.

⁹ Nilikuwa nikizungumza na rafiki yangu mwaminifu sana, si muda mrefu uliopita, ambaye ni Mkatoliki. Naye alisema, “Mungu atauhukumu ulimwengu kwa kanisa Katoliki.” Kama hivyo ndivyo ilivyo, ni kanisa Katoliki lipi? Unaona? Kwa hiyo, kama Yeye akiuhukumu kwa la Methodisti, basi na Wabaptisti je? Unaona? Akiuhukumu kwa moja, hilo lingine limepotea. Kwa hiyo, kuna ghasia nyingi sana hapo.

Lakini inabidi tuliendoe Hilo, ili tupate kujua kauli ye—yetu ya kweli, na Biblia inasema ya kwamba Mungu atauhukumu ulimwengu kwa Yesu Kristo. Na Yeye ni Neno. Yohana Mtakatifu 1, “Hapo mwanzo kulikuwako na Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu.” Na Waebrania 13:8 ilisema, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Nami ninaamini jambo hilo kuwa ni Kweli. Sasa, ninaamini jambo hilo. Katika...

¹⁰ Mungu, hapo mwanzo, akiwa ni Mungu asiye na kikomo; Yeye ana kikomo na... ama hana kikomo, hasa. Sisi tuna kikomo. Nia Yake ni kuu zaidi, nasi, katika nia zetu ndogo zenye kikomo, hatuwezi kufahamu hekima Yake kuu, isiyo na kikomo. Lakini basi, wakati anaposema jambo lolote, linaweza kuwa ni la kushangaza sana kwetu, kumsikia akisema jambo fulani katika Maandiko, bali halina budi kutukia. Ninaamini ya kwamba Maneno Yake hayatapita kamwe. Kwa hiyo, ninaamini ya kwamba Mungu, akijua ya kwamba sisi katika maskini akili zetu zenye kikomo tusingaliweza kufasiri nia. Ya—Yake kuu, Yeye hufasiri Neno Lake Mwenyewe. Hahitaji mfasiri yeyote. Yeye hufasiri Neno Lake Mwenyewe, kwa kuthibitisha Neno hilo katika majira Yake.

¹¹ Ninaamini ya kwamba, Mungu, hapo mwanzo, ya kwamba Nuhu alikuwa Neno kwa siku ile, kwa Ujumbe Wake.

Sasa, aliye fuata, baada ya huyo, akaja Musa. Sasa, Musa asingaliweza kulichukua Neno la Nuhu. Asingeweza kujenga meli na kuwasafirisha majini katika Mto Nile kuwatoa Misri, au kwenda kwenye nchi ya ahadi, ama na mambo kadha wa kadha. Ujumbe wake haukutenda kazi katika siku ya Nuhu; huyo ulikuwa ni sehemu ya Neno la Mungu lillothibitishwa kuwa Kweli na Musa.

Wala Yesu asingeweza kuhubiri Neno la Musa. Na Luther asingeweza kudumisha Neno la kanisa Katoliki. Wesley, asingeweza kudumisha Neno la Luther. Na Wapentekoste, wasingeweza kuchukua Neno la Methodisti. Wao... Unaona?

Kanisa linakua. Kila wakati, umepangwa katika Maandiko hapa. Kwa hiyo, Mungu, kwa Roho Mtakatifu, analifunua Neno Lake, kwa kulidhihirisha na kulithibitisha Yeye Mwenyewe, akionyesha ya kwamba ni Neno Lake likitimizwa katika siku liliyoahidiwa.

¹² Yesu alisema jambo hilo. Yeye alisema, "Msiponiamini Mimi, aminini kazi nizitendazo," kwa kuwa zinashuhudia kuhusu kwamba Yeye alikuwa ni nani, unaona, kama mtu ye yote angaliyajua Maandiko.

Sasa, Yeye alikuja kwa njia ya kipekee sana, ya ajabu sana, hata watu hawakutaka kumwamini, kwa sababu, "Yeye, akiwa Mwanadamu, alikuwa aki jifanya Mwenyewe ni Mungu."

Kwa hiyo, Yeye alikuwa Mungu, kwa sura. "Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake."

"Wala hakuna mtu awezaye kufanya kazi hizi Mungu asipokuwa pamoja naye," kama tunavyojua Nikodemo alisema hayo. Hilo, Baraza la Wazee liliamini jambo hilo.

¹³ Sasa, tunajua jambo hilo, Neno hilo. Laiti wangalilijua Neno! Yeye alisema, "Kama mngalimjua Musa, mngalinijua na Mimi, kwa maana Musa aliandikia habari Zangu." Nasi tunaangalia. Kama wangalikuwa wameangalia huko nyuma katika Maandiko, kuona yale ambayo Masihi alipaswa kufanya, basi wangalimjua Yeye kwa uthibitisho, ya kwamba, "Mungu, kwa njia ya Kristo, alikuwa akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake," na kutimiza ahadi zote zilizomuhusu Masihi, alizokuwa afanye. Yesu alilishuhudia Neno hilo, akilifanya Neno hilo liishi kwa ajili ya siku hiyo.

¹⁴ Nami ninaamini ya kwamba leo tunaishi katika jambo lilo hilo: Mungu akishuhudia Neno Lake, kwa kuthibitisha yale aliye sema Yeye angefanya. Sasa, tunajua ya kwamba hii ndiyo siku ya wokovu, ambapo Mungu anawaita watu kutoka duniani, kutoka katika maisha ya dhambi, kuingia katika maisha ya utumishi. Na katika siku ambayo Mungu ameimwaga Roho

Yake kutoka Juu, ishara kuu na maajabu zinapaswa kufuatana na huduma ya siku hii. Hii ndiyo . . . wakati mvua ya vuli na mvua ya masika zinaponyesha, pamoja. Nasi tunajua ya kwamba kunapaswa kuwa na ishara kuu na maajabu. Ambazo, katika madhehebu mengi makubwa. Hili linakataliwa.

Ila ninashukuru sana kwa ajili ya milango hii iliyofunguliwa ambayo nimeipata, ya kuingilia, na uhuisho ambao vijana wanaume wamepewa kama vile mchungaji wenu hapa. Ambao amewafanya . . . Kwa kuwa ninaanza kuzeeka, na ninajua ya kwamba siku zangu zimekwisha, na ninajua sasa ya kwamba vijana wanaume hawa wanaweza kuuchukua Ujumbe huu na kuendelea kuusambaza upesi hadi kule Kuja kwa Bwana, kama hatakuja katika kizazi changu. Ambapo, ninatumaini kumwona Yeye. Ninamtazamia kila siku, nikikaa macho, nikijitayarisha kwa ajili ya saa hiyo.

¹⁵ Sasa hebu na tuzungumze na Mwandishi kabla hatujakisoma Kitabu Chake, tunapoinamisha vichwa vyetu.

Baba wa mbinguni, tunakushukuru, sisi kuwa hai usiku wa leo, hata kurudi kwenye jiji hili. Tukiwa tumeketi hapa katika mandhari hii ya milima, tukiangalia huko juu na kuona theluji, na maua ya rangi ya machungwa yakichanua, wakati uo huo, ni ulimwengu wa kupendeza jinsi gani uliotupa wa kuishi! Na jinsi ambavyo tunaona ya kwamba mwanadamu amevuruga na—na kufanya katika dunia hii, inatufanya kujionea aibu, Baba.

Tuko hapa, usiku wa leo, kujaribu kutoa jitihada zetu, kujaribu kuwafanya watu waone jambo hili kuu ambalo Mungu amefanya, na kujua ya kwamba kuna kitu fulani kikuu zaidi ukivuka tu kwenda upande wa pili. Jalia tukitarajie hicho, usiku wa leo, Baba, tunapolifungua Neno Lako na kulisoma. Tunaweza kulisoma, baba, bali hebu Roho Mtakatifu na atufunulie Hilo kwa ufunuo. Kwa kuwa tunaomba hilo katika Jina la Yesu. Amina.

¹⁶ Sasa, ninyi ambao mnayenda labda kuandika mihtasari, na—na kusoma Maandiko pamoja na mhudumu, kama—kama vile wanavyolisoma kwa kawaida. Na ilikuwa ni jambo la kawaida, wakati niliponinii . . . miaka kadhaa iliyopita, sikuwa na haja ya kuandika Maandiko yangu, na kadhalika. Lakini nimezeeka kidogo tangu siku hizo. Unaona? Ndiyo kwanza nипите miaka ishirini na mitano, hivi majuzi, miaka ishirini na mitano iliyopita. Kwa hiyo, linakuwa kidogo si jambo zuri. Lakini ningali ninajaribu kushikilia kila kitu ninachojua kufanya katika Neno Lake, mpaka atakaponiita.

¹⁷ Sasa, hebu na tufungue katika Yohana Mtakatifu mlango wa 14, Maandiko yanayo julikana sana ambayo tunataka kusoma usiku wa leo, kutoa katika mlango huu fungu la maneno, Bwana akipenda. Karibu nyote mnajua mlango huu. Inaonekana kuwa, mara nyingi, unatumiwa katika ibada za mazishi. Kama

kulipata kuwa na wakati ambao ningetaka kuhubiri ibada ya mazishi, ingekuwa ni kwa dunia hii. Acha ufe kisha uzaliwe mara ya pili. Yohana Mtakatifu 14:1 hadi 7, ninaamini, nimeweka alama hapa.

*Msifadhaike moyoni mwenu; mnamiwamini Mungu,
niaminini na mimi.*

*Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; . . .
sivyo, ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia
mahali.*

*. . . mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja
tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi
mwepo.*

. . . ninakoenda mwajua njia.

*Tomaso akamwambia, Bwana, sisi hatujui uendako;
nasi twaijuaje njia?*

*Yesu akamwambia, Mimi ndimi njia, na kweli, na
uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi.*

*Kama mngalinijua mimi, mngalimjua na Baba; tangu
sasa mnajua, tena mmewona.*

Bwana na aongeze baraka Zake kwa kusomwa kwa Neno Lake. Nasi tutalirejea tena, wakati tukiendelea, wakati tunapotaka kulizungumzia Kanisa somo dogo.

¹⁸ Jana jioni, nilikuwa huko Yuma; Arizona, yaliko makazi yangu sasa. Mimi—mimi . . . Nilipokuwa hapa kabla sijaishi Jeffersonville, Indiana. Sasa nimekuwa niko huko Arizona, kwa ono lililonipeleka kule, miaka michache iliyopita. Nasi tunaishi kule sasa. Sina kanisa lolote kule.

Ndugu Green, ndugu yetu aliyepo hapa pamoja nasi, ameanzisha maskani ambako ninii . . . moja ya Assemblies of God, kanisa, assemblies ya katikati ya mji. Waliungana, nami nafikiri wote waliambatana na Ndugu Brock na Ndugu Gilmore, wakaliacha kanisa hili wazi. Naye Ndugu Pearry Green, kutoka—kutoka Texas, akaja na kupachukua mahali hapo, ambapo panashirikiana na sisi. Tuna furaha kujua ya kwamba—ya kwamba Ndugu Green amefungua kanisa hili tena lililokuwa limefungwa.

¹⁹ Na jana usiku, nilipokuwa nikihutubia huko Yuma kwa Wafanyabiashara Wakristo, nilizungumza juu ya somo la *Kunyakuliwa*. Sasa, hilo huenda lilikuwa ni somo geni kuzungumzia miongan, kwenye dhi—dhifa, lakini karibu kila mmoja kule alikuwa ni Wakristo. Na hivyo ndivyo ilivyo kwenye ufufuo huu kama huu, ama ka—katika kanisa. Ningeweza kuuliza sasa, “Ni wangapi walio Wakristo?” Pengine kila mkono ungeinuliwa. Wewe ni Mkristo. Na kwa hiyo, kama sisi ni Wakristo, nafikiri kwa namna fulani tunapaswa kujulishwa hilo

kabla ya wakati. Haitupasi kulibunibuni tu. Tunapata taarifa kwamba makusudio yetu yatakuwa ni nini.

²⁰ Nami ninataka kuzungumza juu ya jambo hilo usiku wa leo. Na somo litakuwa: *Mambo Yatakayokuwapo*. Na sasa, nilikuwa nikihutubu jana usiku juu ya *Unyakuo*, kwa hiyo usiku huu, ninataka kuzungumza juu ya somo hili, nipate kuliunganisha pamoja na Ujumbe wa Usiku wa jana. Sasa, kutakuwa na *Unyakuo*, tunajua jambo hilo. Huo uko katika siku za usoni, zijazo.

²¹ Sasa, Yesu hapa anazungumzia, kuhusu, ametangulia kwenda kuntuandalia mahali. "Msifadhaike miyoni mwenu." Sasa, Yeye alikuwa akizungumza na Wayahudi. Kasema, "Sasa, ninyi mmekwisha kumwamini Mungu, niaminini na Mimi. Jinsi mlivyomwamini Mungu, niaminini na Mimi, kwa maana Mimi ni Mwana wa Mungu." Unaona? "Na Mungu," kwa maneno mengine, "Mimi na Baba Yangu ni Mmoja. Baba Yangu anaishi ndani Yangu. Na yale mnayoniona nikifanya, ninayofanya, si Mimi. Ni Baba Yangu anayekaa ndani Yangu. Yeye huzitenda hizo kazi."

"Mungu alikuwa katika Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake."

²² Ilikuwa ni rahisi kwa hao Wayahudi waliokuwa wamefundishwa, katika vizazi na vizazi, kuamini ya kwamba kulikuwa na Mungu mkuu wa mbinguni asiyeonekana. Lakini kuwazia ya kwamba Mungu huyo alikuwa ameshuka na alikuwa akijidhihirisha kupitia kwa utu wa Mwanawе, Yesu Kristo, Mungu aliyejifanya maskani katika mwili wa nyama, hilo lilikuwa kidogo limezidi mno ufahamu wao ku—kuelewa.

Lakini Yeye alisema, "Sasa, kama vile mlivyomwamini Mungu, niaminini na Mimi. Kwa kuwa nyumbani mwa Baba Yangu mna makao mengi, nami ninaenda kuwaandalia mahali." Maisha ya Yesu yalikuwa yakikaribia kwisha, hapa duniani.

Alikuwa amewaonyesha watu, na kuwathibitishia, ya kwamba Yeye alikuwa ni Yehova aliyejifanya mwili, kwa ishara kubwa na maajabu, na katika kurejea kwenye Biblia ambayo alikuwa ameirejea, kujirejea Mwenyewe. Naye alithibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Mungu, aliyejihirishwa.

Sasa Yeye alisema, "Mnapoona maisha Yangu yakimalizika, yanamalizika kwa kusudi fulani. Nami ninaenda zangu, kuwaandalia mahali; ili nilipo Mimi, nanyi mwepo." Yesu kwa hiyo anawaambia wanafunzi Wake ya kwamba maisha haya hayaishii katika mauti.

²³ Sasa, nikisema kwamba hili lilikuwa ni fungu la maneno la mazishi. Kumbuka, sisi, mauti imewekwa dhahiri shahiri mbele zetu, wala hatujui kama huenda kukawa na wengine humu jengoni usiku huu ambao hawataondoka hapa wakiwa hai, katika maisha haya ya kimwili. Hivyo ndivyo jinsi yasivyo na

uhakika. Dakika tano kutoka sasa, huenda ikawa ya kwamba vijana wadogo, wenye afya humu jengoni wanawenza kuwa maiti mnamo dakika tano kutoka sasa. Hiyo ni kweli. Na tena, ingewezekana, katika dakika tano kutoka sasa, sisi wote tungekuwa Utukufuni. Hatujui tu. Hilo limo mikononi mwa Mungu. Yesu alisema Yeye hakujua, Yeye Mwenyewe, wakati huo ungekuwa ni lini, bali, “Hayo yaliwu mikononi mwa Baba peke yake.”

²⁴ Sasa, lakini, Yeye alikuwa akiwaambia, ya kwamba, baada ya mauti kuna kuishi. Kwa sababu, “Ninaenda kuandaa mahali,” hiyo ni kusema, kuwapokea, inaonyesha ya kwamba huko, Yeye alikuwa akizungumza nao, ya kwamba kutakuwa na ku—kuishi baada ya maisha haya kukoma. Na ni faraja ya jinsi gani hilo linapaswa kutupa sisi sote, kujua ya kwamba, baada ya maisha haya kukoma, kuna maisha, tunayoyaendea. Na unapozeeka, hilo linakuwa ni halisi zaidi kwako. Unapoanza kuona siku za maisha yako zikikaribia kumalizika, ndipo unaanza, unaanza kujiandaa vizuri zaidi, ukijitayarisha kwa ajili ya tukio hilo kuu. Ni sasa... Ni mwendelezo wa maisha yaya haya katika ulimwengu mwengine, mahali pengine.

²⁵ Kuzaliwa kwako hapa kuliandaliwa tangu zamani. Nadhani unaamini jambo hilo. Kila mmoja wenu anajua ya kwamba kuzaliwa kwetu kuliandaliwa kabla. Je! ulijua ya kwamba kuwako kwako hapa hakukuanza kama hadithi ya kutunga ama wazo? Kila kitu kilipangwa kabla na Mungu, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ya kwamba wewe ungekuwa hapa. Mungu asiye na kikomo alijua. Na kuwa—kuwa asiye na kikomo, ilibidi ajue kila kiroboto ambacho kingepata kuwa hapa duniani, na ni mara ngapi kingepepesa jicho lake. Huko ni kutokuwa na kikomo. Unaona? Wewe, akili zetu ndo—ndogo, haziwezi kuelewa *kutokuwa na kikomo* Kuna maana gani. Mungu asiye na kikomo, Yeye alijua mambo yote. Kwa hiyo, hakuna kitu kilichoenda kombo.

²⁶ Kama tunajua Neno la Mungu, tunajua mahali tunapoishi. Tunajua saa tunayoishi. Tunajua mambo yaliyo mbele. Tunaona yale tumepitia. Nacho Kitabu cha Mungu ni ufunuo wa Yesu Kristo; kazi Zake katika vipindi mbali mbali nya nyakati, hadi kufikia kwenye kitabu cha Ufunuo, na halafu ahadi Zake zijazo. Kwa hiyo, ahadi Zake zote ni kweli. Mungu hawezu kusema Neno lolote bila ya Hilo Neno kuthibitishwa. Kila Neno analosema halina budi kutimia. Kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu...

²⁷ Watu wengine wanachanganya Mwazo, pale, wakati aliposema, “Mungu hujirudia Mwenyewe.” La. Ni ninii tu, unaelewa vibaya. Unaona?

Mungu, hapo mwanzo, Yeye alisema, “Na iwe. Na iwe. Na iwe.” Ulimwengu ulikuwa ni giza tupu, katika machafuko.

Hata wakati aliposema, “Iwe nuru,” huenda ilichukua mamia ya miaka kabla ya nuru kutoke. Lakini wakati alipolinena, halina budi kutimia. Haina budi kuwa hivyo. Unaona? Naye alinena Neno Lake. Hizo mbegu zilikuwa chini ya maji. Wakati alipoikausha nchi, ndipo hizo mbegu zilipotokea. Asemayo hayana budi kutukia.

²⁸ Yeye alisema, kwa manabii. Nilirejea kwenye jambo hilo jana usiku. Kama, kwa mfano tuchukue Isaya, yeye alisema, “Bikira atachukua mimba.” Ni nani angeweza kuwazia, juu ya mtu aliyeheshimiwa mionganoni mwa watu, kutamka neno kama hilo, “Bikira atachukua mimba”? Lakini kwa sababu yeye . . .

Nabii ni mwakisi wa Mungu. Yeye amefanywa hivi kwamba hawezi kusema maneno yake mwenywewe. Hapana budi iwe ni Maneno ya Mungu anayosema huyo nabii. Yeye ni mwakisi tu, naye ni msemani wa Mungu.

Na kwa hiyo, basi, Yeye alisema, “Bikira atachukua mimba.” Huenda labda asingeweza kuelewa na jambo hilo, bali Mungu alilineni hilo kuititia kwake. Kwa sababu, Yeye aliahidi ya kwamba, “Asinge fanya chochote mpaka amelifunua kwa watumishi Wake manabii.” Ndipo, wakati aliposema hilo, ilikuwa ni miaka mia nane kabla ya hilo halijapata kutimia. Lakini ilibidi litimie.

Hatimaye, Maneno hayo ya Mungu yalitia nanga katika tumbo la uzazi la bikira, naye akachukua mimba na kumzaa Imanueli. “Kwa ajili yetu M—Mtoto amezaliwa, tumepewa Mtoto Mwanamume. Ataitwa Jina Lake, ‘Mshauri,’ ‘Mungu mwenye nguvu,’ ‘Mfalme wa Amani,’ ‘Baba wa milele.’” Hayo yalipaswa kuwa hivyo, kwa sababu Mungu alikuwa amelinena kuititia kinywa cha manabii Wake. Na Maneno yote ya Mungu hayana budi kutimizwa.

Kwa hiyo, tunajua ya kwamba Yesu ameenda kuntuandalia mahali, apate kuwapokea watu Kwake. Kwamba watu hao ni akina nani, natumaini ni sisi tulio sehemu ya watu hao usiku wa leo. Kama sivyo, rafiki yangu, Mungu alifanya njia, hali fulani, kwamba unaweza kuingizwa kwenye hali hizo kama ukitaka. Una uhuru wa kujichagulia. Unaweza kufanya jinsi unavyotaka. Lakini sasa angalia, sasa, katika ulimwengu huu ujao. Kuna ulimwengu ujao.

²⁹ Ni kama tu kuzaliwa kwako hapa, nilisema, wewe ultayarishwa. Mungu alijua wewe ungekuwa hapa.

Na sasa unajua, hata mambo ambayo wazazi wako walifanya, sasa, watu wanafikiri ya kwamba hayo hayapatilizwi kutoka kizazi hadi kizazi, lakini yanapatilizwa.

³⁰ Katika Kitabu cha Waebrania, ninaamini, kwenye kama mlango wa 7, akinena, Paulo pale, hao waandishi, naamini ilikuwa ndio, alikuwa akinena juu ya li—lile tukio kuu lililotukia kwa Ibrahimu, ya kwamba alimtolea zaka Melkizedek,

alipokuwa akirudi kutoka kumpiga mfalme. Na sasa yeye alisema, ya kwamba, "Levi alikuwa katika viuno vya Ibrahimu wakati alipokutana na Melkizedeki, akitoka katika kuwapiga wafalme." Na ndipo alilihesabu hilo kwamba "Lawi akitoa zaka, pia, wakati alipokuwa katika viuno vya Ibrahimu," babu wa babu yake.

Naye huzipatiliza dhambi za watu juu ya watoto wa—wao, kutoka kizazi kimoja hadi kingine, ambaao hawatalitii Neno Lake. Unaona?

³¹ Nyote mliandaliwa kabla na Mungu. Hakuna kitu kinachotukia kwa bahati, kwa Mungu. Yeye anajua yote kuhusu jambo hilo. Yote yamepangwa kabla, yamepangwa kwa vizazi vingi huko nyuma, ili kwamba upate kuwa hapa usiku wa leo. Je! ulijua jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

Hebu wazia, ya kwamba, wewe, wakati mmoja... Nitarudia jambo hili tena. Wewe, wakati mmoja, ulikuwa ndani ya baba yako, katika jeni ya baba yako. Sasa, yeye hakukujua kwa wakati huo, wala wewe hukumjua kwa wakati huo. Lakini, unaona, ndipo tuliwekwa katika tuta, katika tumbo la uzazi la mama, kupitia ndoa takatifu. Na ndipo unakuwa mtu aliyedhihirishwa katika sura kama aliyo baba yako, ndipo kunakuwapo na ushirika.

³² Sasa, njia pekee ya wewe unayoweza kuwa mwana, binti ya Mungu, kwa maana inakupasa kuwa ninii... kuwa na Uzima wa Milele. Na kuna aina moja tu ya Uzima wa Milele, na huo ni Uzima wa Mungu. Aina moja tu ya Uzima wa Milele, huo ulikuwa ni Mungu. Hapo, kuwa mwana wa Mungu, ilibidi uwe ndani Yake daima. Jeni ya Uzima wako, Uzima wa kiroho, usiku wa leo, ulikuwa katika Mungu, Baba, kabla hakujakuwa na molekuli. Unaona? Nawe si kitu ila ni dhihirisho la jeni ya Uzima uliokuwa ndani ya Mungu, kama mwana wa Mungu.

Sasa umedhihirishwa, baada ya Neno Lake kuja ndani yako, kukitia Nuru kizazi hiki. Unadhihirisha Uzima wa Mungu ndani yako, kwa sababu wewe ni mwana ama binti ya Mungu. Kwa hiyo, mnalipata hilo ninalomaanisha? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Unaona? Wewe uko ndani ya... Sasa umedhihirika, umeketi katika kanisa hili, usiku wa leo, kwa sababu kazi yako ni kumdhiihirisha Mungu kwa taifa hili na watu hawa, na ujirani huu ambamo unashirikiana.

Po pote ulipo, Mungu alijua ya kwamba ungekuwa hapa, kwa sababu huna budi kuwa moja ya jeni Zake, au sifa Zake. Ilibidi uwe. Kama ulipata, kama una Uzima wa Milele, basi daima ulikuwa ni Uzima wa Milele. Na Mungu, kabla hapajakuwa na msingi, ulimwengu, alijua ya kwamba ungekuwa hapa. Na wakati Neno, ama maji, "kusafishwa kwa maji ya Neno" ya—yalipokuangukia, lilidhihirishwa katika kitu chenye uhai. Sasa una ushirika pamoja na Baba yako, Mungu, kama jinsi tu ulivyo

nao na baba yako wa duniani. Unaona? Ninyi ni raia wa Ufal-... Si raia, bali ni watoto, wana na binti wa Mungu aliye hai, endapo kama Uzima wa Milele unakaa ndani yako.

Sasa, basi, kama ilikuwa hivyo, Yesu alikuwa ni utimilifu wa Mungu uliodhihirishwa. Yeye alikuwa ni utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili. Kwa hiyo, wakati alipokuja ulimwenguni na akadhihirishwa katika mwili, wewe ulikuwa hapa ndani Yake wakati huo, kwa sababu Yeye alikuwa ni Neno, "Hapo mwanzo kulikuwako Neno; naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu." Neno alifanyika mwili. Kwa hiyo wewe ulitembea pamoja Naye, wakati ulipokuwa ndani Yake, wakati alipokuwa duniani. Uliteseka pamoja Naye, na ulikufa pamoja Naye. Ulizikwa pamoja Naye. Na sasa umefufuka pamoja Naye, na ukadhihirisha sifa za Mungu, umeketi katika ulimwengu wa Roho; tayari umetolewa kwa wafu, umefufuliwa katika Uzima mpya, na umeketi katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu. Loo, hilo linamaanisha mengi sana, siku hizi, enyi Kanisa! Hilo linamaanisha mengi sana kwetu, kujiona tumewekwa mahali petu katika Yesu Kristo!

³³ Sasa, kama sisi ni hizo sifa za Mungu, hatuwezi kuishi kwa kanuni za imani. Hatuwezi kuishi kwa umadhehebu. Inatubidi kuishi kwa Neno, kwa sababu Bibi-arusi ni sehemu ya Bwana Arusi, kama vile mke yeoyote alivyuo sehemu ya mumewe. Kwa hiyo, tunapaswa kuwa hilo Bibi-arusi Neno. Na huyo Bibi-arusi Neno ni nani? Dhhirisho la wakati huu, Bibi-arusi, si kanumi za imani ama madhehebu; bali usia ulio hai wa Mungu, sifa ya Mungu iliyo hai, kuuonyesha ulimwengu sifa za Mungu, katika kuumbwa kwa Bibi-arusi ambaye atadhihirishwa katika wakati huu tunaoishi sasa.

³⁴ Martin Luther asingeweza kudhihirisha sifa tunazodhihirsha, kwa sababu kwamba hayo yalikuwa pale mwanzoni, kule kufufuka, kama vile punje ya ngano iliyoingia ardhini.

³⁵ Sasa, tunanukuu hili tena. Labda mmesoma kitabu hicho, yule Mjerumani aliyekuwa akinidhihaki, na kusema nilikuwa mkereketwa wa dini kushinda washupavu wote wa dini. Yeye alikuwa—alipinga kabisa kila kitu kilichoitwa Mungu, na hata alimdhihaki Mungu. Kasema, "Mungu ambaye angeifungua Bahari ya Shamu na," kasema, "awatoe watu Wake; na akunje mikono Yake juu ya tumbo Lake, na aachilie (katika zile nyakati za giza) watu wote hao wafe na kuteseka, hao watoto wadogo waliwe na simba."

³⁶ Unaona, mpango—mpango wote, Kanisa lote, limejengwa juu ya ufunuo wa Kiungu. Yesu alisema, katika Mathayo Mtakatifu, mlango wa 16, "Mwili na damu havikukufunulia jambo hili, bali Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia jambo

hili." Ilikuwa ni nini? Ufunuo wa Yeye alikuwa ni nani. "Na juu ya Mwamba huu, nitalijenga Kanisa Langu, wala malango ya kuzimu haitalishinda." Unaona?

Ufunuo wa Yesu Kristo katika saa hii; si kile alichokuwa katika wakati mwagine! Kile alichokuwa sasa, Biblia inakidhihirisha. Kinakua katika Bibi-arusi, kufikia kimo kikamilifu. Kwa hiyo, kama punje ya ngano, ya Kristo, ilibidi ianguke ardhini, vivyo hivyo na Bibi-arusi alipaswa kuanguka ardhini, katika nyakati za giza. Punje yoyote inayoingia ardhini haina budi kufa, vinginevyo haitajizaa, kujizaa upya. Nalo lile Kanisa Kuu ambalo Yeye alilianzisha kwenye Siku ya Pentekoste, kwa kumtuma Roho Mtakatifu, ilibidi lipitie kifo cha kishahidi na kuingia mavumbini, kuingia ardhini katika zile zama za giza, kuzaa tena katika wakati wa Luther, na ukae kufikia kimo kikamilifu cha Bibi-arusi wa Yesu Kristo kwa ajili ya siku hii ya mwisho. Unaona? Hakuna njia . . .

³⁷ Kwa hiyo, Bibi-arusi, katika Unyakuo, atatokea. Na hayo yote yamepangwa kabla na Mungu, yote yameungwa mkono. Tangu mwanzo, Yeye alimjua kila mtu, kila mahali, ni nani angeketi, yote kuhusu jambo hilo. Yote yamepangwa mbele. Mungu alijua jambo hilo lingekuwa hapa. Na—na wakati . . . Yeye alilifanya jinsi hiyo, ili kwamba tutakapofika pale. . . Yeye ameenda kutuandalia mahali. Na tutakapofika kule, kila kitu kitakuwa kimeandalialiwa kama tu hata usiku huu wa leo ulivyoandaliwa, kama vile wakati huu ulivyoandaliwa. Naam. Kujua Kwake kukuu hapo kabla kunamwambia mambo yote haya, kwa kutangulia kujua.

³⁸ Yeye yuko mahali pote kwa sababu anajua yote; anajua yote kwa sababu yuko mahali pote. Kwa hiyo, kwa kutangulia Kwake kujua . . . Sasa, Yeye hawezi kuwa tu kama upepo juu ya uso wa nchi, kwa sababu Yeye ni Aliye Hai. Yeye si hadithi tu ya kubuniwa. Yeye ni Aliye Hai. Anaishi. Hata anaishi katika nyumba. Anaishi katika mahali panapoitwa Mbinguni. Na kwa hiyo, kwa kuninii Kwake, akiwa yupo kila mahali; akiwa anajua yote, akijua mambo yote, basi Yeye yupo kila mahali kwa kuwa anajua mambo yote.

³⁹ Wewe, sasa, ulikuua kutoka katika kuzaliwa kwako, ulipozaliwa na kuwekwa katika dunia hii. Mungu alijua ya kwamba ulikuwa uwepo hapa katika dunia hii, nawe ulikuua tangu kuzaliwa mpaka kufikia utu uzima. Mambo ambayo yalioneckana ni ya ajabu sana kwako, katika usichana wako, ujana wako, kama watoto, sasa yanaoneckana halisi sana. Usingewenza kuyaelewa ulipokuwa mtoto. Lakini sasa, kwa kuwa umekuwa mtu mzima, unaanza kufahamu na kuona kwamba kila kitu kilikuwa kimewekwa sawa kabisa. Na, wewe, kweli inamaanisha jambo fulani kwako sasa.

⁴⁰ Hivyo ndivyo ilivyo katika kuzaliwa kwako kiroho. Unafanya mambo usiyoyahamu, wakati ukiwa mtoto mchanga, unakuja madhabahuni. Unayatoa maisha yako kwa Kristo. Unafanya mambo yasiyo kawaida. Unashangaa kwa nini ulifanya hivyo. Lakini baada ya kitambo kidogo, unapokuwa mtu mzima, kama Wakristo waliokomaa, ndipo unafahamu jambo hilo. Unaona? Kuna kitu ambacho kinakua. Unaona ni kwa nini ilikupasa kufanya jambo hilo. Kuzaliwa kwako kiroho! Kuzaliwa kwako kimwili ni mfano wa kuzaliwa kwako kiroho.

Jinsi—jinsi lilivyokufaa, katika maisha haya, ulipokuwa unakua, kila kitu kiliendana vizuri kabisa, kwa sababu ulifanywa kwa ajili ya jambo hilo. Je! halikuwa ni jambo la ajabu, usiku ule ulipoyumbayumba ukaingia katika misheni, ule mkutano wa hema, ama lile kanisa dogo mahali fulani kule pembedni, na kitu fulani mhubiri alihubiri, somo fulani, nawe ulianguka moja kwa moja madhabahuni? Unaona? Unaona? Mungu alijua jambo hilo, kabla ya kuwekwa misingi ya dunia. Unaona? Li—lilioneekana ni jambo geni kwako, kwa nini ulilifanya jambo hilo wakati huo. Lakini sasa unaelewa; ulijua jambo lililotukia. Limeandaliiwa vizuri sana katika maisha haya, na pia itakuwa hivyo katika maisha yajayo. Dunia hii na maisha yake yanaonekana ku—kuendelea unapozidi kukomaa. Kila kitu kinaonekana kikienda sawa kwako.

⁴¹ Siamini katika ninii...ya kwamba eti mtu alitokeea kuwa hapa kwa bahati. Sasa hebu wazia tu, unapokuja u—ulimwenguni, kila kitu kilipaswa kutayarishwa kabla kwa ajili yako, ama kuandaliwa mapema, hasa, kwa ajili yako. Ni vigumu kwangu kufahamu hilo jinsi ambavyo tungeweza kuwazia ya kwamba Mungu ambaye angeweza kutayarisha mambo yote haya mazuri kwa ajili yetu asingeninii...tusingeweza kumtumaini. Kwamba, kama ye ye alituleta katika mchafuko huu tulio ndani yake sasa, na akatutayarishia mambo mazuri ya maisha kwa ajili yetu hapa, ni zaidi sana jinsi gani tunavyoweza kumtumainia kutayarisha mambo yajayo, unaona, mambo ya Milele! Inaonekana, ninasema, ni jambo la ajabu sana.

⁴² Wala si—sidhani ya kwamba Mbinguni ni mahali ambapo mama yangu alikuwa akinisimulia. Ninaamini ya kwamba Kanisa limekomaa zaidi ya hapo. Kuwazia, ilikuwa kwamba, miaka mia moja iliyopita, ama mia mbili, nafikiri watu wa kale walikuwa wakifikiri ya kwamba kila mtu aliyeufu alienda Mbinguni na alikuwa na kinubi, na—na aliketi huko kwenye mawingu na—na kupiga kinubi. Sasa, walijua ya kwamba kulikuwa na mahali palipoitwa Mbinguni. Lakini, wao, kama hivyo ndivyo ilivyo, wanamuziki wote wangetushinda, unaona. Lakini sisi...Lakini si—si mahali pa namna hiyo. Si kupiga vinubi, hata kidogo. Ninaamini, siamini ya kwamba Biblia inafundisha jambo hilo. Lakini hiyo ilikuwa ni dhana waliyokuwa nayo kabla ya utimilifu wa Neno kutokea, ama kule

kufunguliwa kwa ile Mihuri Saba, tulioahidiwa katika wakati huu, jambo ambalo sasa. tunalelewa.

Ninaamini ya kwamba Mbinguni ni mahali halisi, kama tu vile hapa mahali palivyo halisi, unaona, kwa maana Mungu alituanzisha katika malezi yetu ya kiroho katika mahali hapa. Nami ninaamini ya kwamba Mbinguni ni mahali ambapo ni halisi tu kama hapa, ambako hatuketi kule Milele na kuketi tu juu ya wingu. Hatupigi tu kinubi chetu, kote—kote hapa, daima. Lakini tunaenda mahali halisi ambapo tutafanya mambo, ambapo tunaenda kuishi. Tutafanya kazi. Tutapafurahia. Tutaishi. Tunaenda kwenye Maisha, kwenye Maisha halisi ya Milele. Tunaenda Mbinguni, paradiso. Kama tu vile Adamu na Hawa walivyoshughulika, na kuishi, na kula, na kufurahia, katika bustani ya Edeni kabla dhambi haijaingia, tuko njiani tukirudi moja kwa moja kule tena, moja kwa moja, kurudi moja kwa moja. Adamu wa kwanza, kwa njia ya dhambi, alitutoa. Adamu wa Pili, kwa njia ya haki, anaturudisha kutuingiza ndani tena; anatuhesabia haki na kuturudisha ndani.

⁴³ Ninyi watu mmaochukua kanda sasa, juu ya ujumbe wa kuhesabiwa haki, ninataka muuchukue. Nanyi chukueni kanda, ninawataka muuchukue huo. Nilizungumza habari zake, hapa wakati fulani uliopita.

⁴⁴ Angalia jinsi vile wazazi wako wa duniani, kabla hujakuja hapa, kabla hawajajua wewe ulikuwa unakuja, walivyojitayarisha kwa ajili ya kuja kwako. Hebu wazia tu juu ya jambo hilo sasa, wazazi wako wa duniani. Ambaye, mzazi wa duniani ni mfano tu wa Mzazi wa kimbunguni. “Kama tunajua jinsi ya kuwapa watoto wetu vipawa vyema, ni zaidi sana jinsi gani Baba yenu wa Mbinguni anavyojuua kuwapa watoto Wake vipawa vyema.” Yesu alitamka Maneno haya. Unaona?

Walijiandaa kwa ajili ya kuja kwako. Walitengeneza kitanda kidogo, ama wakachukua vidogo, vijiatu, na vijinguo, na kadhalika. Waliandaa, kila kitu kwa ajili yako kuwasili, wakavitayarisha kabla hata hujakuja duniani.

⁴⁵ Yesu ameenda kuandaa kuja kwetu kule. Sasa angalia. “Nyumbani mwa Baba Yangu mna makao mengi.” Ama, hebu tuninii . . .

Simaanishi kuongeza kwenye Neno, wala kutoa Kwake, kwa sababu hatupaswi kufanya jambo hilo. Ufunuo 22 ilisema, “Kila atakayeongeza neno, ama kuondoa Neno kutoka Kwake.” Lakini hebu niseme hili, si kama kuongezea, bali ni ku—kuleta jambo fulani tu.

“Katika Nyumba ya Baba Yangu kuna aina nyingi za majumba makubwa ya fahari.” Siamini ya kwamba tutakopofika Mbinguni kwamba tutakuwa, kwamba kila mtu atafanana tu kabisa na mwингine. Siamini ya kwamba—ya kwamba wote watakuwa na nywele na ngozi nyeupe, ama nywele

nyeusi na ngozi nyeusi, ama—ama wadogo, ama—ama wote ni wakubwa, ama—ama wote ni mapandikizi ya majitu.

Ninaamini ya kwamba Mungu ni Mungu anayependa vitu vya aina mbalimbali. Ulimwengu unathibitisha jambo hilo. Yeye ana milima mikubwa na milima midogo. Ana nyanda. Ana majangwa. Ana vitu mbalimbali, kwa kuwa alivifanya jinsi alivyovitaka. Naye alifanya majira: kiangazi, majira ya baridi, majira ya kuchipua, majira ya kupukutika majani. Alifanya majira. Inaonyesha ya kwamba Yeye ni Mungu anayependa vitu vya aina mbalimbali. Yeye alikuumba wewe wa tofauti na mwingine. Watu wengine wana kiburi sana, wengine ni wagumu kupindukia; na wengine ni wachangamfu; wengine ni wakarimu. Na unapata watu mbalimbali wa kila namna, na ndivyo ilivyo katika Ufalme Wake. Unaona?

⁴⁶ Hebu mwangalie Mtakatifu Petro, na umlinganishe na Andrea. Unaona? Andrea ni yule shujaa wa maombi, alidumu magotini mwake sikuzote. Na mtume Petro alikuwa mmoja wa wale vinga vya moto ambaye alihubiri, na—na kadhalika. Na Paulo alikuwa zaidi sana kama msomi, zaidi sana kama . . . kama nabii, ama kitu fulani, na alijitenga.

⁴⁷ Na, unaona, Musa aliandika Vitabu vya kwanza vinne vya la Kale. Ambapo, yeye aliandika Agano la Kale. Hivyo vingine vilikuwa ni torati, na wafalme, na zaburi, na kadhalika, na yale mtu fulani aliandika juu ya manabii. Lakini Musa aliandika torati, vitabu vya kwanza vinne vya Biblia: Mwanzo, Kutoka, Mambo ya Walawi, na Kumbukumbu la Torati.

⁴⁸ Na halafu Paulo aliandika Agano Jipy. Hiyo ni kweli. Mathayo, Marko, Luka na Yohana waliandika matendo ya yale yaliyotukia, na kadhalika. Lakini Paulo alitenganisha torati na neema, na kuiweka mahali pake. Unaona? Yeye alikuwa ndiye mwandishi wa Agano Jipy. Alitupa maandiko ya Agano Jipy, akiliweka Neno la Mungu katika utaratibu.

Sasa angalia, *mengi*, “majumba mengi makubwa ya fahari,” majumba makubwa ya fahari ya aina nyangi.

⁴⁹ Kama vile, vilima vya aina nyangi; kama vile, mito ya aina nyangi, vijito, maziwa. Hayo yalikuwa hapa ulipokuja, kwanza, kwa sababu wema wa Baba yako wa Mbinguni uliyaweka hapa. Kwa sababu, watu wengine wanapenda milima. Watu wengine wanapenda mito. Wengine wanapenda majangwa. Kwa hiyo, unaona, kuja kwako, Yeye aliju tabia yako na kile ungekuwa, kwa hiyo aliyafanya jinsi tu ambavyo ungeweza kuyafurahia. Loo! Nafikiri huyo ni Baba mzuri sana, unaona, kujua ya kwamba aliyafanya jinsi hii.

Ninafurahi kwamba Yeye aliumba milima. Na—napenda milima. Mimi . . . Nami na—naipenda hiyo. Ambapo, wengine, “Loo, siwezi kuvumilia . . . Loo, hapana shaka Yeye alimaliza kasha lake la mota kule.” Vema, aliimaliza kusudi nipate

kuifurahia. Unaona? Kwa hiyo basi wao wanasema, “Ninapenda nyanda, ambako ninaweza kuona mbali sana.” Vema, tabia mbili mbalimbali, sote wawili tukiwa ni Wakristo.

Lakini Baba alijua ya kwamba wewe ungekuwa hapa, naye akatayarisha kila kitu kwa ajili yako kabla hujafika hapa. Amina. Kuja kwako mara ya kwanza, hapa, Yeye alitayarisha hilo kwa ajili yako wakati ulipofika hapa. Hilo si ni la ajabu sana kuwazia yale aliyofanya?

⁵⁰ Sasa, sasa, lakini kumbuka, hizi ni karama tu zisizodumu, katika mfano. “Sasa, tunajua ya kwamba Musa, katika kuijenga ile maskani jangwani, ama kuitayarisha, yeye alisema alikuwa amefanya mambo yote kulingana na utaratibu wa ile aliyoona Mbinguni.” Unaona? Kwa hiyo, mambo ya duniani yanaonyesha tu jinsi mambo ya Milele yalivyo. Na kama dunia hii tunamoishi leo, ikiwa ni kubwa sana, kama tunavyoipenda; na tunavyopenda kuishi, na kuvuta hewa, na kuona maua na kadhalika; kama—kama hiyo, kama hii hapa ndiyo dhihirisho, ile inayokufa inadhihirisha tu ile iliyo ya Milele. Unapouona mti ukipambana, kuvuta, ukijaribu kuishi, hiyo inamaanisha kuna mti mahali fulani usioshurutika kufanya hivyo.

Unapomwona mtu hapa, akipambana apate kuishi, mtu fulani hospitalini, ama kitanda cha wagonjwa, ama akiwa kwenye ajali, akijitahidi, na mkoromo wa kufa uko kooni mwao, na kuvuta, na kulia, na kuyalilia maisha kwa sauti kuu, hiyo ina maana gani? Kuna mahali, mahali fulani, kuna mwili usiopambana na kulilia hayo. Unaona? Huo haufanyi hivyo kamwe.

⁵¹ Sasa, hizo ni karama zisizodumu kwetu, vitu hivi, vikidhihirisha tu ya kwamba kuna Moja ambapo ndiyo iliyo ya Milele. Hiyo ndiyo Yesu ameenda Zake kuntuandalia, ile iliyo ya Milele kwa ajili yetu. Sasa, vinadhihirisha tu kuna kubwa zaidi ya namna hiyo, kwa sababu hivi ni vya aina ile ile.

⁵² Sasa, kumbuka, Biblia ilisema, “Kama maskani hii ya makao yetu, kama ikiharibika, ikiangamia, tuna moja tayari inayongojoa.”

Kama tu vile mtoto mchanga, misuli yake midogo, ndani ya mama yake, inavyojinyonganyonga na kujigeuza. Na, lakini ninii tu... Unaona? Nawe unaona, unawenza kumchukua mwanamke, kama alikuwa anafofa sana; bali anapokuwa mja mzito, punde kidogo kabla mtoto huyo hajazaliwa, kuna wema fulani unaomzunguka mama huyo. Fika karibu naye, daima kuna kitu fulani, ni mpole zaidi. Kwa nini? Kuna roho ndogo ya malaika inayongojea kuupokea mwili huo wa maumbile ya kawaida. Mara tu anapozaliwa, pumzi ya uhai inamwingia. Ndipo Mungu anaipulizia humo ndani yake, naye anakuwa nafsi iliyo hai. Sasa, punde tu mtoto huyu mchanga anapozaliwa, papo hapo mwili wa kiroho upo hapo kumpokea.

Na sasa, wakati mwili huu unapozaliwa hapa, katika dunia hii, kama vile ambavyo mtoto mchanga anapozaliwa, kuna pia mwili usiopatikana na mauti unaongojea kuipokea roho hiyo ndani yake tena. Loo, ni jambo kuu jinsi gani! Tuko—tuko sasa ndani ya Kristo Yesu, (amina), watoto wachanga, watoto wachanga katika Kristo, watoto wa Mungu, tukingojea ukombozi mkamilifu, wakati wa Kuja kwa Bwana wetu Yesu, ninii... kutupokea Kwake juu, wakati mwili, huu uharibikao, utakapochukua kutokuharibika.

⁵³ Mfano, mambo yote aliyofanya, hudhihirisha mambo yajayo. Kama tu vile mwili unavyokupa hapa, kama tu vile mwili huu, aliokupa wewe wa kuishi ndani yake, unaonyesha tu ya kwamba kuna mmoja ulio mkuu zaidi, bado, ujao. Unaona? “Kama tukichukua, ama tumechukua sura ya ule wa duniani, pia tutachukua sura ya ule wa Mbinguni,” ambaodhauna maovu katika huu ujao. Sasa, huu unabeba uovu, magonjwa, mauti, huzuni. Nimeeleza hapa tu, si muda mrefu uliopita, nikihubiri juu ya *Jinsi Neno la Mungu Linavyobadilisha*, kuhusu vile kwamba—kwamba mwili huu, una uovu ndani yake.

⁵⁴ Na ustaarabu huu wote wa kisasa tunaoishi ndani yake ni wa Ibilisi. Hamwamini jambo hilo? Biblia inasema iko hivyo; ulimwengu huu, kila serikali. Hatutaki kuamini jambo hilo. Bali Biblia inanena jambo hilo dhahiri, ya kwamba kila serikali, kila ufalme wa dunia hii, ni mali ya Ibilisi na unatawaliwa na Ibilisi. Yesu alichukuliwa na Shetani, juu, na kuonyeshwa falme zote za ulimwengu zilizokuwako, zitakazokuwako, na kadhalika. Naye Shetani alizidai, kwamba ni zake, wala Yesu hakubishana naye, kwa sababu yeye ni mungu wa dunia hii. Unaona? Naye akasema, “Nitakupa Wewe hizo kama utanisujudia na kuniabudu.” Unaona? Yeye alikuwa akitaka kumpa Yesu hizo, bila dhabihu. Unaona? Alikuwa akipiga bei Naye.

Bali ulimwengu ulikuwa umetenda dhambi. Kwa hiyo, mshahara wa dhambi ulikuwa ni mauti, Naye imbidi kufa. Hiyo ndiyo sababu Mungu alidhihirishwa katika mwili, kusudi apate kuchukua mauti juu Yake, apata kulipa deni. Hakuna kitu cha kurudi. Hakijatiwa alama. Imelipiwa kabisa, kabisa. Deni yote imelipiwa. Ni mali Yake sasa. Na sisi ni wajumbe wa Ufalme Wake, tuliokusanyika hapa pamoja usiku wa leo, katika Jina la Yesu Kristo Mfalme wetu, tukiketi katika ulimwengu wa Roho.

⁵⁵ Sasa, katika ulimwengu huu tunaoishi, elimu hii. Ninataka kuwathibitishia. Elimu, sayansi, ustaarabu, na mambo haya yote ambayo inaonekana tunayafurahia siku hizi, ni ya Shetani, na yataangamia. Unasema, “Ndugu Branham, ati ustaarabu?” Naam, bwana. Ustaarabu huu ulisababishwa na Shetani. Mwanzo 4 inathibitisha jambo hilo. Mwana wa Kaini, unaona, alianzisha ustaarabu huu, akijenga miji, na vinanda, na kadhalika. Na ustaarabu ulikuja kwa njia ya maarifa. Maarifa

ndiyo Ibilisi aliyomwuzia Hawa, katika bustani ya Edeni, ambayo yalimfanya kubanwa, kuvunja amri za Mungu.

Kwa hiyo kutakuwa na ustaarabu katika ulimwengu ule tunaouendea, bali hautakuwa ni ustaarabu wa aina hii, kwa kuwa katika ustaarabu huu tuna magonjwa, huzuni, tamaa mbaya ya uzinzi, mauti, kila kitu katika ustaarabu huu, kibaya. Lakini katika ustaarabu ule hakutakuwa na yoyote ya mambo haya. Hatutahitaji sayansi.

Sayansi ni upotovu wa kile cha asili, hata hivyo. Unaona? Unaatua molekuli, kuatua atomi na kufanya *hivi na vile*, kukulipua wewe. Unachukua baruti, unagonga *hiki*, kuua kitu fulani. Unachukua gari. Na kutoa petroli kutoka ardhini, na mali ghafi kutoka ardhini, kulegeza uimara, kusudi dunia ilipuke. Na mtu unaendesha barabarani maili tisini kwa saa, na kumwua mtu. Unaona? Loo, wasiwasi wa jinsi gani, msongamano, na kuharakisha; inatubidi kusukuma, na kuiba. Loo! Unaona? Yote ni ya Ibilisi.

Ufalme wa Mungu hautakuwa na motokaa, ndege, wala mafanikio yoyote ya sayansi. La. Hautakuwa na elimu yoyote, hata kidogo. Itakuwa ni elimu ya hali ya juu sana kuliko hii, hata hii haitakumbukwa. Unaona? Elimu, ustaarabu, na yote haya, yanatokana na Shetani.

Sasa, unasema, “Ndugu Branham, kwa nini unasoma, basi?”

⁵⁶ Unaona, ni kama tu, ni kwa nini ninavaa nguo sasa? Katika ustaarabu uliokuwa ukija, uliokuwa wa kwanza, hawakuhitaji nguo zozote. Walikuwa wametiwa utaji. Hawakuwa na sababu ya kuva nguo, kwa kuwa hawakujua walikuwa uchi. Sasa u-... Sasa unaona, ya kwamba, wakati huu, basi, ya kwamba tunajua ya kwamba tuko—tuko—tuko—tuko uchi, dhambi inadumu hapa, basi inatupasa kuva nguo. Lakini haikuwa hivyo hapo mwanzo; hakukuwa na dhambi. Unaona?

⁵⁷ Sasa, jambo lile lile liko katika suala la ustaarabu, kwa jumla. Tunasoma. Tunaandika. Tunafanya jambo hili. Lakini kamwe usizamie kwenye jambo hilo. Kamwe usilifanye kuwa ni mungu wako, kwa kuwa huyo ndiye mungu wa ukomunisti. Unaona? Si la Yesu Kristo.

⁵⁸ Yesu Kristo ni kwa imani; si yale unayoweza kuthibitisha kisayansi, bali ni yale unayoamini. Siwezi kukuthibitishia kisayansi, usiku huu, katika jengo hili, ya kwamba kuna Mungu, lakini hata hivyo ninajua Yeye yuko hapa. Lakini, kwa imani yangu, minathibitisha hilo.

Ibrahimu asingeweza kukuthibitishia kisayansi ya kwamba atampata mtoto kwa mwanamke huyo, naye akiwa na umri wa karibu miaka mia moja. Bali imani yake ilithibitisha jambo hilo. Unaona? Hakuhitaji thibitisho lolote la kisayansi. Mbона, ninii... Mbона, daktari angalisema, “Huyo mzee ana kichaa, amekuja hapa akisema ya kwamba atampata m—mtoto kwa

mwanamke yule; yeye akiwa na umri wa miaka mia moja; na mkewe tisini.” Lakini, unaona, Mungu alisema hivyo, kwa hivyo halihitaji sayansi. Inahitaji imani, kuliamini Neno la Mungu, si sayansi.

⁵⁹ Kwa hiyo, shule zetu na kadhalika ni hasara. Kwa kuwa, Mungu kamwe hakusema, “Enendeni mkajenge shule,” ama hata, “Muwe na shule za Biblia.” Mnajua jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ye ye alisema, “Hubirini Neno.” Hiyo ni kweli kabisa. Mifumo yetu ya elimu imetupeleka mbali zaidi na Mungu kuliko kitu chochote nijuacho, hiyo ni kweli, mbali sana na Mungu. Si kujenga shule, hospitali, na kadhalika; hilo lilikuwa ni kwa ajili ya walimwengu na kwa kundi hilo. Lakini, sina kitu dhidi yao, yana nafasi zao, bali hilo bado silo.

Tunajenga hospitali, nzuri sana, na kutumia madawa mazuri sana tulio nayo, na maelfu wanakufa humo kila siku. Lakini, loo, jamani, katika Ufalme wa Mungu, hakuna kufa, hakuna huzuni. Amina. Hakuna haja ya mambo haya ya dunia. Lakini tumepita kutoka katika jambo hili, tukaingia katika ukweli wa Mungu; pale ambapo tunakazana sana kujaribu kupata mambo, kwa sayansi. Na jinsi tunavyozidi kuwa wa kisayansi, ndivyo tunavyozidi kujiletea vifo vingi. Tunapigana vita vya bure katika hayo, kwa hiyo achaneni nalo. Na kwa imani, mwaminini Yesu Kristo Mwana wa Mungu, usiku wa leo, na mumkubali. Ye ye Ndiye.

⁶⁰ Sayansi inakutayarishia kitu gani? Vifo zaidi. Hiyo ni kweli. Masputniki na kila kitu kinarushwa juu, mambo haya yote, kusambaza mauti na kila kitu kote duniani. Usitumainie jambo hilo. Geuza kichwa chako ukielekeze juu zaidi ya kitu hicho, kuelekea Mbinguni. Angalia mahali Yesu anapoketi, “Katika mkono wa kuume wa Mungu,” usiku wa leo, “akiishi daima kutufanyia upatanisho tunapokiri.” Kukiri nini? Ya kile tunachoamini. Neno Lake kuwa ni Kweli.

⁶¹ Sasa, tunaona, maisha haya yana kila namna ya uovu, kwa hiyo basi maisha yajayo hayatakuwa nayo. Haya yana tamaa mbaya za mwili, na magonjwa, mauti. Kwa sababu, ni kitu gani? Siyo hiyo nyumba aliyoenda kuandaa. Hii ni nyumba ya maradhi. Ni wangapi wanaojua nyumba ya maradhi ni kitu gani? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hakika. Vema, hiyo ndiyo unayoishi ndani yake. Nyumba ya maradhi ni mahali wanapowaweka watu wote waliopatwa na magonjwa. Vema, hivyo ndivyo hasa dhambi inavyotufanyia, imetuweka katika nyumba ya udongo yenye maradhi. Kama ulininii... Wasingemruhusu mtu mwingine ye yote kuingia katika nyumba ya maradhi, kwa maana kuna kila namna ya vijidudu vinavyoruka kila mahali mle, na—na watu wataambukizwa vijidudu hivi na—na kuwa wagonjwa, wenyewe. Nayo dhambi ilitingiza katika nyumba ya maradhi ya Ibilisi.

⁶² Loo, bali hiyo nyingine inaitwa, “Nyumba ya Baba Yangu.” “Naenda kuwaandalia mahali. Kuwatoa kwenye nyumba hii ya magonjwa na kuwapeleka katika Nyumba ya Baba Yangu.” Amina. Haya basi; niwatoe katika nyumba hii ya kale ya udongo yenye maradhi. Yeye ameenda kutuandalia mahali, mahali pakamilifu ambapo hapana maovu, hapana maradhi, hapana uzee, hakuna mauti.

Ni mahali pakamilifu pakiwaita kwenda kwenye ule ukamilifu, nawe inakubidi kuwa mkamilifu upate kufika kule. Biblia ilisema hivyo. Yesu alisema, “Iweni basi wakamilifu, kama vile Baba yenu wa Mbinguni alivyuo mkamilifu.” Ni Ufalme mkamilifu, kwa hiyo hapana budi iwe ni watu wakamilifu watakaokuja. Kwa sababu, inakubidi kusimama na kuolewa na Mwana wa Mungu aliye mkamilifu, nawe huna budi kuwa Bibi-arusi mkamilifu. Kwa hiyo unawezaje kufanya jambo hilo kupitia jambo lingine lolote ila Neno kamilifu la Mungu, ambalo ni, “Maji ya farakano, yanayotusafisha na dhambi zetu”? Amina. Hiyo ni kweli. Damu ya Yesu Kristo, wazia jambo Hilo, inayotiririka, Neno lililojaa Damu. Amina. Ile Damu, Ne—Neno la Mungu likitoka Damu, ya kumwoshea Bibi-arusi. Amina. Naam, bwana. Yeye anasimama akiwa mkamilifu, bikira, asiyeghoshiwa. Hajawahi kutenda dhambi kamwe, kwanza. Amina. Alinaswa katika jambo hilo. Unaona?

Hiyo hapo Nyumba ya Baba aliyoenda kuandaa.

⁶³ Hii ilitokana na kujuana kimwili, na kutokana na kuanguka, na haina budi kuanguka pamoja na kule kuanguka. Haidhuru utakitia viraka jinsi gani kitu hicho cha kale, kitaanguka, kwa vyovyote vile. Kimekwisha, kwa sababu kimehukumiwa, kwa sababu Mungu alisema hivyo. Kimekwisha. Mungu yuaenda kukiangamiza. Alisema hivyo. Kutakuwako na kufanya upya kwa kitu hicho chote. Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

Hapo mwanzo, wakati dunia ilipozaliwa, wakati Mungu alipoyarudisha maji nyuma, kwanza, kutoka ardhini, kama alivyofanya kwa yale maji kutoka katika tumbo la uzazi la mama, dunia ilizaliwa. Naam. Na watu wakaanza kuishi juu yake wakati Mungu alipowaweza mle. Na ndipo wakaanza kufanya dhambi. Basi ilibatizwa, kwa kuzikwa majini, katika siku za Nuhu. Kisha ikatakaswa kwa Damu ya Muumba ikiidondokea juu yake.

Na sasa hiyo ndiyo namna unavyokuja wewe, kupitia kuhesabiwa haki, kwa kumwamini Mungu. Ulibatizwa kwa toba, ama, pia, kwa ondoleo la dhambi zako. Ulitubu dhambi zako mbele za Mungu, Naye akakusamehe kwazo. Nawe ukabatizwa, kuonyesha ya kwamba ulikwisha, ulikwisha kusamehewa; ukikiri kwa watu, na kuonyesha ulimwengu, ya kwamba unaamini ya kwamba Yesu Kristo alikufa kwa ajili

yako. Nawe... alipachukua mahali pako, na sasa unasi mama mahali Pake. Yeye alifanyika wewe, upate kufanyika Yeye.

Ndipo nguvu za Mungu zinazotakasa ziliosha tabia zote kuziondoa katika maisha yako. Ulikuwa ukivuta sigara, ukinywa pombe, ukifanya mambo yasiyokuwa mazuri, ukisema uongo, kila kitu. Ndipo nguvu za kutakasa za Damu ya Yesu Kristo zinaingia maishani mwako na kuondoa mambo yote kutoka kwako. Ikitokea useme kitu si kibaya, upesi sema, "Ngoja kidogo. Samahani. Sikutaka kusema hilo namna hiyo." Unaona? Ibilisi ana mtego uliotegwa pale. Lakini una neema ya kurudi, kama wewe ni Mkristo halisi, sema, "Nilikosea." Naam. Kwa maana, kwa sababu hiyo, sasa, ninii...

⁶⁴ Sasa, jambo la pili ulilopokea, lilikuwa ni ubatizo wa Roho Mtakatifu na Moto.

Sasa, Mungu, wakati utawala huu wa miaka hii Elfu Moja utakapomalizika, Mungu ataupa ulimwengu huu ubatizo wa moto. Utakilipua kitu hicho chote. "Mbingu na nchi zitawaka moto." Petro alisema hivyo. Na kitu hicho kitapata ubatizo wa moto, kufanya upya kwa kitu hicho chote. Na ndipo kutakuwako na mbingu mpya na nchi mpya. Hiyo ni kusema, wakati, ambapo haki inadumu.

Hapo ndipo tulipo. Tumetoka kuwa viumbe vinavyopatikana na mauti, kutoka viumbe vyta wakati, kuwa viumbe vyta Milele. Wakati Neno la Mungu lilipoziwasha nafsi zetu, nasi tukawa wana na binti za Mungu, tukiwa na zile sifa, jeni ya Mungu ikiwa ndani yetu, kuwa wana na binti za Baba, Mungu aliye Mbinguni, tukilia, "Aba, Baba! Mungu wangu, Mungu wangu, katika Nyumba ya Baba yangu."

⁶⁵ Sasa, ulimwengu huu wa kale hauna budi kuanguka, kwa maana ulikuja kupitia kwa kujuana kimwili. Na ulipitia katika uasi, hapo mwanzo. Na sisi tulizaliwa hapa kwa tendo la kujuana kimwili, kupitia kule kuanguka, na hauna budi kurudi moja kwa moja kwa njia hiyo hiyo, kwenye kule kuanguka. Lakini ule ambaao Yeye sasa anauandaa kwa ajili yako, hauwezi kuanguka, kwa sababu anaufanya kuwa hivyo. "Nimeenda..."

Vipi kama ingalitubidi kukaa katika mwili wa namna hii? Hivi huna furaha kuna kitu kama mauti? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa si hilo ni la ajabu? Lakini sasa, tuseme, kwa mfano...

Miaka michache iliyopita, nilikuwa mvulana mdogo, na sasa mimi ni mtu wa makamu. Nina rafiki yangu anayeketi moja kwa moja pale, Bw. Dauch, naye ana umri wa miaka tisini na mitatu, siku chache zilizopita. Hebu mwangalie sasa. Miaka arobaini ama arobaini na mitano zaidi, huyo ingekuwa ni mimi. Sasa weka miaka mingine arobaini juu yake. Ungeenda wapi? Kitu pekee...

⁶⁶ Nina furaha ya kwamba kuna kitu cha kututoa katika nyumba hii ya maradhi. Kuna mlango uliofunguliwa, nao unaitwa mauti. Yesu anasimama kwenye mlangoni huo. Amina. Yeye ataniongoza kuvuka mto. Yeye atanipitisha kwenye mlango huo. Kuna mlango mkubwa uliosimama kule, unaoitwa mauti. Na kila wakati moyo wako unapopigapiga, wewe uko pigo moja karibu na huo. Na siku moja sina budi kuufikia huo mlango. Huna budi kufika pale. Lakini nitakapofika pale, sitaki kuwa mwoga. Sitaki makelele na kughairi. Ninataka kufika kwenye huo mlango, nijifunike kwa mavazi ya haki Yake (si yangu), Yake.

Kwa jambo hili ninajua, ya kwamba, “Ninamjua Yeye katika nguvu za kufufuka Kwake.” Kwamba, atakapoita, nitatoka mionganini mwa wafu, kuwa pamoja Naye, kutoka katika nyumba hii ya maradhi. Mahali po pote mwili huu huenda utaanguka, na po pote utakapoangukia, cho chote kile, nitatoka siku moja, kwa sababu Yeye aliniahidi Hilo. Na tunaamini jambo hilo. Naam, bwana. Yeye anaufanya Mmoja usioweza kuanguka.

⁶⁷ Angalia jinsi mama mjamzito, duniani siku hizi, jinsi ambavyo mwili wa mama unavyotamani vitu fulani. Ninazungumzia, nakisia na kutumaini, kwa watu wote wazima watakaofahamu. Mama, katika kuzaliwa kwa mtoto mchanga, kama kuna kitu kinachokosekana mwilini mwake, huanza kutamani kitu fulani. Angalia jinsi ambavyo baba...

Ninakumbuka tulilewea, kama familia maskini, na—na karibu hatukuwa na kitu cha kula tulipokuwa watoto wadogo. Wengi wenu mliteseka kwa jambo lile lile.

Kwa hiyo jinsi ambavyo, wakati, kabla ya watoto hawajazaliwa, mama angetamani kitu fulani. Na baba angetafuta kila mahali, kila kitu, apate kumpatia hicho. Unaona? Ni ninii wake, mwili, mwili wake, kalisi na kadhalika ya mwili wake, na vitaminini anazohitaji. Kadogoo anaumbwa, unaona, naye anatamani sana vitu, vyakula vya mtoto ajaye. Na jinsi ambavyo, wazazi, wanajaribu kukipata ili kwamba mtoto azaliwe kikamilifu na mwenye furaha iwezekanavyo. Unaona jinsi ambavyo wazazi wako watafanya jambo hilo? Wakati kuna kitu kinachohitajika, mama anashuhudia jambo hilo, unaona, mfumo wake umewekwa sawa. Mnaelewa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kwamba, jinsi ambavyo wakati kuna kitu fulani kinachohitajika hapa, kwa ajili ya mtoto ajaye, ma—mama anaaza kukitamani sana hicho.

⁶⁸ Sasa, hebu simama kwa muda mfupi. Ni kwa nini tuna miamsho? Ni kwa nini tunakusanyika pamoja? Ni kwa nini daima ninawakaripia watu? Ni kwa nini ninawahimiza ninyi wanawake wa Kipentekoste, “Acheni kujipaka rangi, kujipodoo, na kukata nywele zenu, na vitu kama hivyo”? Ni kwa nini ninasema jambo hilo? Ni kwa sababu, njia ya mtindo wa

kale ya kipentekoste haikuwa na tabia ya kufanya jambo hilo. Njia halisi ya Biblia si kufanya hivyo. Ninyi mnaovaa hizi kaptura na nguo zinazowapasa wanaume, je! mnajua ya kwamba Biblia inasema ya kwamba ni chukizo kwa Mungu? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Lakini tunaruhusu jambo hilo. Ni kwa nini Roho Mtakatifu anashikilia kukemea? Anajua kuna kasoro fulani pale. Lazima tuwe katika kimo kikamilifu cha Yesu Kristo. Inatupasa kuwa wana na binti za Mungu. Sharti kutenda kama watoto wa Mungu.

⁶⁹ Muda mrefu uliopita, hadithi moja fupi ilisimuliwa. Nilimwona ndugu mmoja mweusi ameketi kule nyuma. Huko kusini, walikuwa wakiuba watumwa. Na jambo hili, walipokuwa na watumwa kule, wakati utumwa ulipokuwa unaendeshwa, kabla ya ukombozi wa watumwa, wa lile tangazo. Na wangepitia kule na kuwanunua, hao watu, kama vile wangenunua ga—gari la mitumba, mfanyakibashara. Walikuwa na risiti, na kuwauza hao wanadamu kama tu walikuwa—walikuwa ni magari ya mitumba. Ulipata risiti za kuwanunua.

⁷⁰ Wakati mmoja mnunuzi alifika pale, wakala. Naye alikuwa akienda kuninii... Yeye angezunguka katika haya mashamba makubwa na kuwanunua watumwa. Ndipo akafikia kwenye shambu moja kubwa ambamo walikuwa na watumwa wengi, naye alitaka kuona walikuwa wana wangapi. Na wote walikuwa huko nje, wakifanya kazi. Nao wa—walikuwa na huzuni. Walikuwa mbali na nyumbani. Walikuwa wametoka Afrika.

Walikuwa wamewaleta huku. Makaburu waliwaleta huku na kuwauza kama watumwa, na kwa hiyo walikuwa na huzuni. Walijuwa kamwe hawatarudi nyumbani tena. Wangeishi na kufia humu nchini. Nao walikuwa, mara nydingi, wangebeba mijeledi na kuwacharaza. Walikuwa ni mali ya huyo tajiri, naye alifanya nao aliyataka. Na walininii tu... Kama alikiua kitu hicho, alikiua. Na kama yeye, chochote kile, alikifanya tu. Huo ni utumwa, kama vile Israeli ilivyokuwa, na—na wengi wa mataifa walikuwa wameletwa katika utumwa. Nao ingewabidi kuwachukua maskini watumwa hao. Walitumika tu. Walikuwa wakilia, unajua, wakati wote, na wenye huzuni.

⁷¹ Lakini waliona mmoja wa hao watumwa, kijana, alikuwa amevimbisha kifua mbele, kichwa chake kimeinuka juu namna *hiyo*. Haikulazimu kumcharaza. Haikulazimu kumwambia la kufanya. Kwa hiyo huyo wakala akasema, “Nataka kumnunua mtumwa *yule*.”

Akasema, “Hauzwi.”

Akasema, “Ningetaka kumnunua.”

Akasema, “La. Hauzwi.”

Kasema, “Je! yeye ndiye bosi wa hao wengine?”

Kasema, “La.” Kasema, “Yeye si bosi. Ni mtumwa.”

Akasema, "Vema, labda unamlisha tofauti na vile unavyowalisha hao wengine."

Kasema, "La. Wote wanakula huko nje kwenye manchani, pamoja."

Akasema, "Ni kitu gani kinachomfanya mvulana yule tofauti sana na hao wengine?"

Akasema, "Hili hapa jambo moja. Nilishangaa kwa kitambo kidogo, pia. Lakini mvulana yule, mgeni kutoka Afrika, bali huko Afrika baba yake ndiye mfalme wa kabilia lake. Na, ingawa, yeze ni mgeni aliye mbali na nyumbani. Anajiheshimu kama mwana wa mfalme. Yeye anajua ya kwamba, huko ng'ambo ya nchi, ya kwamba baba yake ndiye mfalme wa kabilia lake. Na sasa yeze anajiheshimu, kwa sababu anajua yeze ni mwana wa mfalme."

⁷² Loo, ndugu, dada, wewe na mimi, katika ulimwengu huu tunaoishi, hebu na tujiheshimu kama wana na binti za Mungu. Sisi ni wageni hapa, bali matendo yetu yanapaswa kuwa ni kulingana na amri za Mungu, ya kwamba sisi ni wana na binti za Mungu. Tabia yetu, tunapaswa kuenenda na kufanya, na kila kitu, kulingana na amri zilizowekwa na Mungu.

"Na ni chukizo kwa mwanamke kucaa vazi linalompasa mwanamume." Ni vibaya na ni dhambi, "Kwake kukata nywele zake," Biblia ilisema hivyo, "haimpasi hata kuomba."

Unasema, "Na *hili je?*"

⁷³ Mtu fulani alinifuatilia; mhudumu mkubwa, anayejulikana sana, si muda mrefu uliopita. Kasema, "Ndugu Branham, njoo. Ninataka kukuwekea mikono." Kasema, "Wewe utaiharibu huduma yako."

Nikasema, "Ati nini?"

Kasema, "Kuwakemea hao watu namna hiyo."

Nikasema, "Ninawaambia ninii . . ."

Akasema, "Ninaamini jambo hilo." Kasema, "Mimi ni Mpentekoste, pia. Ninaamini ya kwamba wanawake hawapaswi kukata nywele, hawapaswi kujipodoa, na vitu kama hivi jinsi wanavyofanya, kujipodoa nyuso zao rangi." Kasema, "Hawapaswi kufanya hivyo. Lakini," kasema, "Mungu alikuита kwa ajili ya kuwaombea wagonjwa."

Nikasema, "Aliniita kuihubiri Injili." Naam.

Naye akasema, "Ninaamini jambo hilo. Lakini," kasema, "unafikiri hivyo?"

Nikasema, "Naam. Angalia mliyo nayo, mipango yote hii mikubwa, televisheni, na chochote kile. Mimi sina kitu ila Mungu nitakayewajibika Kwake." Hiyo ni kweli. Nikasema, "Sina kitu ila Mungu nitakayewajibika Kwake."

Akasema, "Na—na—na . . . Utaua huduma yako."

Nikasema, “Huduma yoyote itakayouwawa na Neno la Mungu, inapaswa kuuwawa.” Hiyo ni kweli. Hakika. Hiyo ni kweli kabisa.

Akasema, “Vema, utaiuwa.”

⁷⁴ Nikasema, “Ni nani atakayelisema basi? Unaona? Mtu fulani hana budi kulisema. Mtu fulani hana budi kushindania yale yaliyo Kweli, haidhuru inaumiza jinsi gani.” Nanyi ndugu, mtu kama Mkristo, kama watu wanaoamini ya kwamba tunaenda Mbinguni, Roho Mtakatifu Mwenyewe atatuonyesha katika mfano katika Neno la Mungu.

Akasema, “Unajua unalopaswa kufanya?” Kasema, “Watu wanakuamini wewe kuwa ni nabii.” Kasema, “Unapaswa kuwa unawafundisha wanawake hawa jinsi ya kupokea karama za unabii na mambo kama hayo, na mambo makubwa, mambo ya juu zaidi badala ya jambo dogo.”

⁷⁵ Nikasema, “Nitawafundishaje aljebra wakati hata hawawezi kujifunza ABC zao? Wakati hata hawataweza kufanya jambo la kawaida, unaona, jambo la kawaida, utawaambiaje mambo ya juu?” Wakati hata hutaanza kutoka ninii... Unataka kufikia mwishoni mwa ngazi kabla hujafikia hatua ya kwanza. Hiyo ndiyo sababu unaanguka. Unaona?

Lakini fika hapo chini, na uendeele kupanda moja kwa moja jinsi Mungu anavyokuongoza juu. Unaona? Rekebisha maisha yako na daima ufuate kila sehemu ya Neno ambalo Mungu amekuteua kulifanya.

⁷⁶ Sasa wazia jinsi ambavyo Mungu... Tunapaswa kuwa na mwenendo mzuri na kutenda kama Wakristo. Matendo yetu yanapaswa kuwa kama ya Wakristo. Kwa sababu, sisi ni wageni hapa. Haya sio makazi yetu. La. Tumewekwa tu hapa, kwa muda kidogo. Inabidi kuondoka, kila mmoja wetu, usiku wa leo.

⁷⁷ Sasa wazia. Kama Mungu, katika rehema Yake, anamfanya mama, kabla ya mtoto mchanga kuzaliwa, anatamani sana vitaminii fulani, na maneno ya mama yanasema, “Baba, ni-ni-ninataka tikiti, ama tikiti maji. Ninataka kitu fulani, ama kingine.” Hakipatikani... Mbona, atafanya yote awezayo, kupata hicho, kwa sababu anajua ya kwamba anataka mtoto wake azaliwe akiwa mkamilifu iwezekanavyo. Unaona? Naye atafanya kila kitu awezacho kufanya, kukipata.

⁷⁸ Ni zaidi sana vipi Yeye anavyoweza, kukipata! Yeye ni Muumba. Sasa wazia jinsi alivyo na uwezo, kutuandalia mwili, kuishi kama mwili Wake Mwenyewe wenye utukufu, kama tunataka kuishi. Kuna kitu fulani ndani yetu, kinachohitaji, kuishi. Na kuna kitu ndani yetu kinachotaka kufanya yafaayo. Ndipo Mungu atamwita mtu fulani jukwaani, ama mimbarani, atakayehubiri Ukweli mtupu. Kwa nini? Unaona? Inakuonyesha. Ndipo, kama wewe ni mwana halisi wa Mungu, unaanza kupiga kelele, “Mungu, liondoe *hilo* kwangu. Nitahiri jambo *hili*.

Niondolee mambo *haya*.” Kwa nini? Linahitajika kwa ajili ya Makazi yako ya Mbinguni unayoyaendea, ambako ametangulia kwenda kutuandalia. Unapaswa kuwa Bibi-arusi Neno halisi wa Kristo.

⁷⁹ Nilikuwa nikihubiri siku chache usiku zilizopita juu ya dhabihu, katika siku za upatanisho. Nilikuwa nikihubiri juu ya mahali pekee ambapo Mungu, Kanisa pekee ambalo Mungu atakutana na mwanadamu humo, na ambalo liko, Yeye alisema, mahali ambapo aliweka Jina Lake. Yeye alisema, “Sitakutana nao mahali pengine popote ila mahali hapo, lango ambalo niliweka Jina Langu ndani yake.” Sasa, Yeye hakutani na wewe katika lango la Kimethodisti, lango la Kibaptisti, ama lango la Kipentekoste, ama lolote la hayo. Bali aliweka Jina Lake katika Mwanawee. Yeye alisema, “Nilikuja katika Jina la Baba Yangu.”

Mtu yejote huja, na mtoto yejote, huja katika jina la baba yake. Yeye . . . Nilikuja katika Jina la Branham, kwa sababu baba yangu alikuwa ni Branham. Nawe unakuja katika jina lako kwa sababu hilo lilikuwa ni jina la baba yako.

Na Yesu, Mwana, alikuja katika Jina la Baba. Naye alisema aliweka Jina Lake, “Katika lango hili nililoweka Jina Langu, hiyo ilikuwa ni ile dhabihu.” Na ndani ya Yesu Kristo ndipo mahali pekee ambapo utapata ushirika na kumwabudu Mungu.

Unasema, “Vema, mimi ni mfuasi wa kanisa.” Hilo halileti tofauti yoyote. Unapaswa kuwa katika Kristo.

Mhudumu fulani wa kimadhehebu, hivi majuzi usiku, aliniambia, kasema, “Bw. Branham, angalia hapa. Yesu alisema, ‘Yeyote aaminiye.’ Biblia ilisema, ‘Yeyote aaminiye ya kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, amezaliwa na Roho wa Mungu.’”

⁸⁰ Nikasema, “Hivi biblia haisemi pia, ya kwamba, ‘Hakuna mtu awezaye kumwita Yesu Kristo, ila kwa Roho Mtakatifu?’” Unaona? Huwezi kuifanya Biblia iseme uongo. Inapaswa kushikamana moja kwa moja.

Kwa hiyo huna budi kuzaliwa mara ya pili hasa, kwa Roho Mtakatifu kuwa ndani yako, ambaye anashuhudia, wewe mwenyewe, unajua ya kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu. Na basi kama umezaliwa, na u sehemu; kama wewe ni mwana wa Mungu, katika Neno la Mungu; unawezaje kulikana Neno? Roho Mtakatifu anawezaje kukufanya uamini kanuni ya imani, kwamba inakubidi kufanya kitu kama *hiki*, wakati Biblia ilisema jambo lingine fulani? “Inatubidi kujiunga na kanissa, na kufanya jambo *hili*, ama kufanya jambo *lile*,” wakati Biblia inakwambia dhahiri la kufanya? Unaona? Na wakati unapoona jambo Hilo, nawe unaruka moja kwa moja na kuingia ndani Yake, ndipo uko Nalo moja kwa moja. Endelea tu kusonga moja kwa moja mbele, nalo linakua tu.

Kama vile se—se—seli zazi inavyoingia katika tumbo la uzazi la mwanamke pamoja na yai. Na basi wakati yai hilo dogo linapoanza kukua, na kuanza kuleta seli zazi nyingine, halileti seli zazi moja ya binadamu, na seli moja ya mbwa, na seli moja ya ng'ombe. Linatoa seli zote za kibinadamu.

⁸¹ Na wakati mwana wa Mungu, wakati ile iliyochaguliwa tangu zamani... Hilo ni neno baya la kutumia, bali ni Mungu. Hii Hapa Biblia ya Mungu. Kujua kabla kwa Mungu kunaweza kuchagua tangu zamani, kufanya kila kitende kazi kwa ukuu Wake. Wakati ile mbegu iliyochaguliwa tangu zamani, uliyopaswa wewe kuwapo, na Mungu akakuita, na maskini hiyo mbegu ya kifaranga cha tai mle ndani iliposikia Neno la Mungu, itajenga juu yake, Neno moja juu ya lingine, juu ya lingine, juu ya lingine. Haitachanganyikana na kanuni yoyote ya imani.

⁸² Angalia. “Katika malango haya, kila siku, wanapaswa kula kosha mpya. Na hakutakuwa na chachu itakayoonekana mionganoni mwao, katika zile siku saba.” Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Zile nyakati saba za kanisa, basi, hakuna chachu, hakuna kanuni ya imani, hakuna kitu chochote kitakachoongezwa. Haina budi kuwa ni mkate usiotiwa chachu kabisa. “Chachu yo yote isionekane mionganoni mwenu, hata kidogo.” Chachu pekee, Neno lenyewe, ni hilo peke yake. Nalo Neno hilo ni Mungu. Naye Mungu alifanyika mwili, katika Utu wa Yesu Kristo, ambapo, hilo ndilo hilo Lango. “Hilo ndilo Lango nitakapokutana na ninyi hapo ndani, kuabudu, mtakapozifuata amri za Mungu.”

⁸³ Kwa hiyo, kama wewe umeninii, usiku wa leo, umekuja tu, useme, “Ninamtolea Yesu Kristo maisha yangu,” nawe kamwe hujapata kumpokea Roho Mtakatifu; ingia ndani Yake. Huna budi kufanya jambo hilo. Huna budi kukua ndani Yake. Mwombe Mungu kulundika Neno juu ya Neno, namna hiyo, mpaka uwe kimo kikamilifu cha mwana wa Mungu, ama binti ya Mungu.

Kuyachukua mambo ya ulimwengu? Yohana wa Kwanza unasesma, “Ukiipenda dunia, au mambo yaliyomo duniani, ni kwa sababu kumpenda Mungu hata kakumo ndani yako.” Umedanganywa. Una upendo wa ulimwengu humo, na umekudanganya, Ibilisi amekudanganya, kwa kuyarundika mambo pale, akionyesha. Unaona? Huwezi... Vema, basi, huwezi kuondoa Neno moja la Mungu kutoka katika Biblia.

Ni kitu gani kilisababisha dhambi ya kwanza? Si kwa uongo mkubwa wa dhahiri, bali ni kwa sababu Hawa alielewa vibaya, Ibilisi alimpotosha, Neno moja. Neno moja, lilikata mnyororo, na akakataa kuchukua Neno moja. Huo ulikuwa ni mwanzo wa Biblia.

Yesu alikuja katikati ya Biblia. Alisema, “Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha

Mungu.” Hilo ni Neno lote la Mungu. Je! mnaamini *Hilo* ndilo ufunuo Wake? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Neno lote la Mungu.

Halafu, katika Ufunuo 22, Yesu alikuja kwa Yohana, katika kisiwa cha Patmo. Basi Yesu, “Mimi Yesu nimemtuma malaika Wangu kushuhudia mambo haya.” Unaona? “Kila atakayeondoa Neno moja kutoka kwenye Hiki, ama kuongeza neno moja Kwake, nitamwondolea sehemu yake katika Kitabu cha Uzima.”

⁸⁴ Siyo kusema tu, “Vema, ni—ninamwamini Yesu Kristo, Mwana wa Mungu.” Hilo ni sawa. Basi ongeza hayo mengine. Unasema, “Nimehesabiwa haki. Ninampa mhudumu mkono wangu. Ninamwamini Yesu Kristo.” Basi huna budi kuzaliwa mara ya pili. Huna budi kujazwa na Roho Mtakatifu. Unaona? Endelea tu kuongeza, unapodumu kuendelea. Unakua katika kimo cha mwana na binti wa Mungu. Jamani!

Mungu, akiwa tayari kututayarisha, na kutupa ile shauku maishani mwetu, ya kwamba tunataka kuona kitu fulani. Ni wangapi hapa ndani wanamtaka Mungu zaidi? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mbona, inaonyesha kuna Mungu zaidi kwa ajili yenu. Unaona? Mnaonea shauku sana hilo. Maumivu yenu madogo ya utungu wa kuzaa yanakuja. Unaona? Mniamhitaji zaidi, kusudi tupate kuwa na furaha, na huru, na wakamilifu. Hatuna budi kuwa.

⁸⁵ Kama vile ile—ile ninii ndogo—maskini ile seli zazi ya uhai inavyokuwa ninii... kifuani mwa Mungu, kama tu, na hiyo seli zazi ya uhai imo kifu—... kifuani mwa mama. Mungu anakuza; na anaenda, ameenda kutuandalia mahali, mahali pa Milele pamoja na Yeye Mwenyewe; si mahali ambapo pana nyumba ya maradhi, panapokufa, dhambi, uzinzi, na uchafu wa duniani hapa. Kama moyo wako uko kwenye hayo, inaonyesha ya kwamba kamwe hajakutana na Mungu. Unaona? Umechochewa. Una fikira za uongo.

Unajiunga tu na kanisa na kusema, “Vema, mimi ni mfuasi wa hili. Mama yangu alikuwa mfuasi wa hilo.” Huenda hilo lilikuwa ni sawa katika siku za mama yako, bali tunaishi katika siku nyingine.

⁸⁶ Ujumbe wa Wesley kamwe usingalininii... Yeye kamwe asingemchukua Luther. Luther aliamini katika kuhesabiwa haki, bali Wesley alikuwa na kutakaswa. Wapentekoste walikuja, wasingeweza kuchukua kuhesabiwa haki tu, kutakaswa. Wao, ilikuwa ni wakati wa kurudishwa kwa zile karama. Sasa sisi tunaondoka kwenye hizo. Unaona?

Zile hatua tatu za M—Mzabibu ukikua. Ya kwanza, ni jani dogo, Luther akatokea, kutoka katika yale matengenezo. Vema. Hayo yalikuwa ni shina. Angalia maumbile. Mungu na maumbile hufanya kazi katika mwendeleo, kwa sababu Mungu yuko katika maumbile. Unaona? Halafu kukaja kishada, chavua,

wakati wa Kimethodisti. Ndipo wakaja Wapentekoste, loo, jamani, ni kamilifu kabisa, unaona, kama tu punje ya ngano inavyoonekana kana kwamba ni ngano kamilii, punje ya ngano. Ifungue, hakuna ngano pale, hata kidogo. Ni kapi, bebaji Lake, bali Uhai huo unatenda kazi mle wakati wote. Unaona?

⁸⁷ Hao waliokuwa huko nyuma katika wakati wa Luther wanamkubali Luther. Uhai huo ulipita, bali ulienda na kuunda madhehebu. Punde si punde unajua, likawa ni kundi la madhehebu ambalo mwisho wake ni kuchomwa moto. Unaona? Shina linakauka; ni bebaji tu. Baadhi yao wangali wanajaribu kukaa kwenye lile shina bebaji la kale, hawajui kitu kuhusu Mungu, wamekuifa. Wao wanasema, “Vema, angalia, sisi ni jani. Tulikuwa katika Luther.” Hiyo ni kweli. Lakini angalia mahali lilipo sasa. Unaona?

“Sisi tulikuwa ni Wamethodisti.”

Na hata, “Sisi tulikuwa ni Wapentekoste.” Lakini waangalie Wapentekoste, jinsi walivyokuwa baridi na wa kawaida, jinsi ambavyo kila mtu anaondoka anaenda Zake. Unaona? Ni kitu gani? Ilikuwa ni bebaji la Mbegu halisi. Unaona? Haya mengine yote yalikuwa ni bebaji, bali yaliunda madhehebu. Kama ukisema, “Mimi ni Mpentekoste.” Hilo halimaanishi kitu cha zaidi kwa Mungu kuliko kama ungalisema ulikuwa Mkatoliki wa Kirumi ama Myahudi, ama chochote ungeweza kuwa.

⁸⁸ Huna budi kuzaliwa, Uhai huo unaopitia kwenye bebaji hilo pale. Usikae katika shina. Usikae kwenye Mbegu. Nenda moja kwa moja mpaka kwenye sehemu iliyo kamilifu.

⁸⁹ Sasa, kumbuka, na kila matengenezo tuliyokuwa nayo, kwa hao Walutheri wote na kadhalika, katika miaka mitatu wanaunda madhehebu. Hiyo ni kweli. Kila ufufuo uliunda madhehebu katika miaka mitatu.

Wazia jinsi huu umechukua muda mrefu kiasi gani, miaka ishirini na kitu, wala hakuna madhehebu. Kwa nini? Ni Mbegu, inakuja, ikiumbika chini ya ganda, namna *hii*. Kuanikwa, sasa inapaswa kuanikwa katika Uwepo wa Mwana, ipate kuiva kuwa punje yenyе utukufu kama Ile iliyoingia kwanza. Kanisa halisi lililoingia ardhini, kwanza, lineariti moja kwa moja kuititia kwenye shina, lipate kutokea, Kanisa lingine, wakati kivuna nafaka kitakapokuja kuiokota. Uhai ulioshuka ukaingia ndani ya Luther, Uhai ulioingia ardhini katika Methodisti, Uhai ulioingia ardhini katika Upentekoste, utaingia katika punje. Wote utaingia moja kwa moja katika punje, na kutoka, ukifanya Mwili mkamilifu wa Yesu Kristo.

⁹⁰ Kama tu vile juu linavyochoomoza, asubuhi. Huwezi kuangalia maumbile yoyote isipokuwa yanashuhudia juu ya Mungu. Huhitaji hata Biblia, kujua ya kwamba kuna Mungu. Maskini juu linazaliwa, likiwa mtoto mchanga mdhaifu. Yapata saa moja, linaenda, linaenda shulenii. Saa nne au saa tano,

limetoka. Adhuhuri, liko kwenye nguvu zake zote. Saa tisa alasiri, linaanza kuzeeka. Saa moja ama mbili, thenashara... Saa kumi na moja ama thenashara alasiri, mgongo unaanza kuinama. Linakufa. Je! huo ndio mwisho wake? La. Linafufuka tena kesho yake asubuhi. Uhai, mauti, kuzikwa, kufufuka!

⁹¹ Angalia majani yakiota mtini. Yanachipua, majani mazuri, ya kupendeza; yanaleta kivuli; yanaza tunda lake. Halafu, muda si muda wajua, msimu wa kupukutika majani unaingia, unayafikia, mauti; unakimbia chini kwenye mizizi, unaingia ardhini tena. Je! huo ndio mwisho wake? Msimu wa kuchanua unarudi moja kwa moja tena kushuhudia. Loo! Huo ni uhai unaodumu.

Lakini, ndugu, dada, sisi tuna Uzima wa Milele. Tuna Uzima wa Milele kupidia kwa Huyu mkuu aliyekuja, ameenda, anaweza kutuandalia mwili. Na maumivu haya yote tusikiayo kwenye misuli na viungo, kama vile ninyi wanawake mnavyojisikia mmehukumiwa na yale mnayofanya, ninyi wanaume mnaojishikilia kwenye mafundisho ya seminari, na kadhalika, nyote mnataka kusema, "Ni—ninakariri kanuni hii ya imani. Ninafanya jambo *hili*." Lakini kuna kitu fulani kilicho ndani yako kabisa, unapoona macho ya vipofu yakifunguliwa; viziwi wakifaha...vipofu. Mambo haya yote yaliyoahidiwa. Unaona Neno likihubiriwa katika nguvu Zake. Unamwona malaya, toka mtaani, akifanywa mama wa kuheshimika. Unaona m—mlevi akitoka pale, na kuwa mtakatifu halisi wa Mungu. Jamani! Unaona? Kuna jambo fulani, Uzima mle ndani. Nawe unaanza kujisikia, "Vema, labda sipaswi kufanya jambo hilo." Lakini, unaona, kitu ni kwamba, ni kitu fulani. Mwili wako una njaa ya haja fulani, basi, "Fanya hima." Lakini Mungu ana vitamini papa *Hapa* ndani kwa kila sehemu ya Mwili huo. Yesu ameenda kutuandalia mahali kifuani mwa Mungu; naam, bwana, seli fulani zazi ndogo, mwana wa Mungu, mwana mdogo ama binti mdogo wa Mungu.

⁹² Yesu aliomba jambo moja tu, katika ombi Lake kwa Baba. Unajua lilikuwa ni nini? Jambo moja, baada ya dhabihu yake yote aliyotoa hapa duniani, maisha aliyoishi, njia aliyofuata. Aliomba jambo moja. "Kwamba nilipo Mimi, nao wawepo." Yeye aliomba ushirika wetu. Hicho ndicho kitu pekee alichomwomba Baba katika maombi, ushirika wenu milele. Kama ukitaka kusoma jambo hili katika Yohana 17, na kifungu cha 24. Basi tunapaswa kumhitaji jinsi gani? Kama yeye anatamani...

Sasa sikilizeni. Kama kweli umezaliwa na Roho wa Mungu, hilo linamaanisha kila kitu kwako. Unaona? Si kitabu fulani cha sheria. Huishi sheria zozote na kadhalika. Unaishi kwa neema ya Mungu, Roho ya Mungu.

⁹³ Mara nyingi nimesema jambo hili. Kama mmishenari, Ningekuwa nikisafiri nchi za ng'ambo. Vipi kama nilimwita

mke wangu ndani, watoto wangu, "Sasa angalieni hapa, ninyi watoto! Sikilizeni hapa, Bibi Branham! Mimi ni mumeo. Usiwe na wanaume wengine wakati nimeondoka. Ukifanya hivyo, nitakuchuna ngozi nitakaporudi nyumbani"? En-he. Unaona?

Niponde mguu wangu chini kwa kishindo, "Ninyi watoto, mnasikia ninayosema?"

"Naam. Ndio, baba. Naam, baba."

"Hebu nisikie tu ukosefu wowote wa adabu? Unaona?" Unaona? Sasa, hiyo kweli ingekuwa ni nyumba ya jinsi gani?

Sasa vipi kama yeye akisema, "Sasa, umemaliza, bwana? Sasa ninataka kukwambia jambo fulani. Bw. Branham, mimi ndiye mke wako halali wa ndoa! Usiwe na rafiki wengine wowote wa kike na wewe pia, uko safarini"? Sasa, hiyo itakuwa si ni nyumba kweli kweli? Sasa, hicho kingekuwa ni kitu.

Hatufanyi jambo hivyo. Ninampenda, naye ananipenda. Anapojuja ya kwamba ninaondoka, anajua siendi Mungu asiponiita kwenda. Tunapiga magoti chini, na kuwakusanya watoto. Tunaomba. Nilisema, "Mungu mpPENDWA, mlinde maskini mwenzangu, watoto wangu." Wao wanasema, "Mungu, mlinde baba wakati tumeondoka, akiwa safarini." Ndipo wakati tunapoenda huko . . .

⁹⁴ Sasa, vipi kama nikifanya jambo baya huko? Vipi kama nikifanya maovu, nifanye jambo baya? Na nirudi na kumwendea maskini mke wangu, nisimame pale na kuuangalia uso wake unaoingia makunyanzi, na nywele zake zinazoanza kuota mvi, nikamwendea pale na kusema, "Mpenzi, ninataka kukwambia jambo fulani. Unajua ya kwamba ninakupenda."

"Hakika, Bill, najua unanipenda."

⁹⁵ "Hebu nikwambie niliyofanya. Nilichukua msichana fulani nikampeleka nyumbani." Ni—niseme, "Je! utanisamehe kwa jambo hilo?" Ninaamini angenisamehe. Kweli ninaamini. Lakini je! ningefanya jambo hilo? Wakati nikiangalia, akisimama pale, ninaona hizo nywele zikianza kuota mvi, na kujua ya kwamba amesimama kati yangu na watu wote, nami ninajua jinsi amekuwa mke halisi, ningeweza kufanya jambo hilo? Afadhalii nife kuliko kumuumiza. Afadhalii nife.

Na huo, katika upendo wa fileo kwa mke wangu, ni zaidi jinsi gani upendo wa agapo kwa Mungu! Loo, nisingefanya jambo lolote kumwudhi Yeye. Hapana kwa kweli. Ni—ninampenda. Ninataka kufanya kila kitu ambacho Yeye—Yeye anataka nifanye. Ninataka kutimiza kila Neno ambalo yeye alilosema, haidhuru ulimwengu unasema nini. Wao, hawataamini jambo Hilo, hata hivyo. Ninataka kujua yale yeye aliyoniambia kufanya. Na kama nikikosa kitu fulani, ninataka anipe. Na kumwishia, tukijiepusha na ulimwengu.

⁹⁶ Maskini mwili huu wa kale una ninii zake...Hebu niwaambie. Mwili huu wa duniani unaowazia mengi sana, ambao unaulinganisha na Hollywood. Unautunza sana. Hautakuwako muda mrefu zaidi. Wewe kumbuka. Umesikia ule unabii, ambao Bwana alinipa, "Unazama." Naam, bwana. Angalia. Utazama. Hebu angalia tu. Sasa, hajapata kuniambia jambo lolote lisilo kweli, bado. Nitachukua hilo kwa mtu ye yote anayetaka kusema. Sijui ni lini ama ni wapi, lakini umekwisha. Hukumu inaning'inia juu yake. Hakuna ukombozi kwa ajili yake; umepita. Unaona?

⁹⁷ Sasa angalia jambo hili. Ishi kwa ajili Yake, tukijiepusha na ulimwengu. Sasa angalia. Unaangalia kwenye televisheni, baadhi yenu akina dada, nanyi mnashuka kwenda hapa na mnataka, ninyi wasichana. Ninyi ni vijana. Mnajua jambo hilo. Lakini ninyi ni Wakristo. Mnaona? Ninyi mko tofauti. Hamtaki kuwa kama dunia. Mnaipenda dunia. Si ninyi vijana tu; baadhi yenu ninyi wazee. Unaona? Vema, ni kitu gani kinachofanya jambo hilo? Unaona? Mnaangalia televisheni, mnashuka kweda dukani, mnaona maskini nguo hizi ndogo chafu ambazo wanawake wanavaa, ambazo ni mbovu.

Mnajua kitakachotukia katika Siku ya Hukumu? Unaweza ukawa msafi tu kwa mume wako uwezavyo kuwa, bali katika Siku ya Hukumu itakubidi kuwajibika kwa kufanya uzinzi. Yesu alisema, "Kila amwangaliaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha kuzinzi naye moyoni mwake." Ni nani wa kulaumiwa? Wewe. Unaona? Ulijianika, kaptura na suruali.

Wanawake fulani waliniambia, si muda mrefu uliopita, wakasema, "Mimi sivai kaptura, Ndugu Branham. Ninamshukuru Bwana kwa ajili ya jambo hilo. Ninavaa suruali."

⁹⁸ Nikasema, "Hizo ni mbaya zaidi." Ni mbaya zaidi. Hiyo ni kweli.

⁹⁹ Hata huwezi kununua gauni, ni vigumu, kwa ajili ya wanawake. Akasema, mwanamke mmoja alisema, "Vema, ulisema kweli. 'Huwezi. Huwezi kuipata'" Lakini wangali wanauzu vitambaa na wana vyerahani. Unaona? Kwa hiyo hakuna kujitetea, hata kidogo. Unaona? Unaona?

Inaonyesha, dada. Mimi ni ndugu yako. Nami ni mtumishi kwa Kristo, ambaye itabidi kuwajibika kwenye Kiti cha Hukumu kwa yale ninayosema hapa usiku wa leo. Unaona? Utasimama, ukiwa na hatia ya kufanya uzinzi, kwa sababu kwamba upendo wa Mungu umevuja ukatoka moyoni mwako. Ungali unaenda kanisani. Unaweza ukawa unacheza katika Roho. Unaweza ukawa bado unanena kwa lugha. Na mambo hayo ni mazuri, bali hayo bado Sie. La, bwana.

¹⁰⁰ Kumbuka, Biblia ilisema, "Katika siku za mwisho kutatokea Makristo wa uongo," si Yesu wa uongo. Wasinjewumilia jambo

hilo. Bali, "Makristo wa uongo," wapakwa mafuta wa uongo. Wamepakwa mafuta kabisa na Roho, na Roho Mtakatifu, na wangali ni wa uongo. Unaona? Kuna wawili . . .

¹⁰¹ Wewe ni watu watatu. Huo wa nje ni mwili. Una hisi tano, ambazo unawasili ana na mwili wako wa duniani nazo. Ndani ni roho. Kuna hisi tano hapo, upendo na dhamira, na kadhalika, unawasili ana. Bali ndani ya hiyo ni nafsi.

¹⁰² Kumbuka, "Mvua huwanyeshea wenye haki na wasio haki." Mvua ile ile itakayoifanya punje ya ngano kukua hufanya gugu kukua pia. Unaona? Ni kitu gani? Ndani ya mbegu hiyo kuna asili fulani, na asili hiyo huonyesha, hujionyesha yenye. Inaweza kuwa katika shamba lile lile, pale pale pamoja na gugu. Gugu na ngano zipo pamoja, zinafurahi vivyo hivyo. Kichwa chake kimeinama chini. Inakufa kwa njaa ya maji. Mvua inapokuja, gugu linaweza kupaza sauti kwa nguvu kama tu ngano iwezavyo. "Bali kwa matunda yao mtawatambua." Unaona?

¹⁰³ Enyi Wakristo, huenda nisiwaone tena. Unaona, ni miaka mingi tangu nilipokuwa hapa. Huenda nisiwaone tena. Lifuateni Neno la Mungu. Jiangalieni kwenye kioo.

Kama maskini mvulana mmoja wakati mmoja, alikuwa huko kijijini, hajawahi kamwe kuona kioo. Alikaa kwenye nyumba ya shangazi ya—yake. Alianza kupanda vipandio. Akaona kioo, naye akaona mvulana mdogo ndani ya kile kioo. Akaendelea kutembea, akiangalia. Na—naye angepunga mkono, mvulana huyo mdogo naye angepunga. Basi akaendelea kuangalia. Hajawahi kujiona kwenye kioo. Kwa hiyo alipokikaribia vyakutoshya, akageuka, akasema, "Mbona, Mama, yule pale ni mimi!"

¹⁰⁴ Unaonekanaje, katika kioo cha Mungu? Je! kinaakisi binti ama mwana wa Mungu? Je! kuna kitu fulani, ambacho, ukisikia Hicho, je! kinakufanya umchukie mtu anayesima? Ama, je! kuna kitu fulani kinachovuta, kusema, "Ninajua mtu yule anasema kweli kwa sababu hilo liko kwenye Maandiko"? Basi, hizo ndizo vitamini zinazohitajika kwa ajili ya mwili huu uliokusudiwa kuwako kule, nyumba ambayo ule mwininge utahitaji utakapofika kule. Unaona? "Nyumba hii; kama tumechukua wa duniani."

¹⁰⁵ Sasa kumbukeni, tunautukuza sana mwili huu. Tunauvalisha nguo nyingi sana. Tunafanya mambo mengi, ambayo, si ya lazima, kubadili nguo baada ya nguo baada ya nguo, takataka zote hizo. Na—na, loo, kila mtu tu!

Hebu acha tu mtu fulani anaanza kitu fulani. Mtu paka vipandio vyako rangi nyekundu basi waone akina Jones wakivipaka vyao rangi nyekundu. Hebu badilisha kutoka Chevrolet ununue Ford, nao kamwe hawawezi kuvumilia jambo hilo. Ni wakati wa watu kujilinganisha na wengine. Hebu

ninii... Acha mwanamke fulani aje kanisani, amevaa namna fulani ya kofia, waangalie wanawake wote wakiinunua hiyo; hasa mke wa mchungaji, unaona, hebu angalia tu jambo linalotukia. Sasa, hilo ni kweli. Huo ni ukweli kabisa. Ni wakati wa watu kujilinganisha. Ndugu, unapaswa kuwa ni wakati wa kujilinganisha. Na hao wote—mambo hayo yote ni—ni kwa kusudi fulani.

Sijali kama koti langu linafanana na suruali yangu ndefu. Nami nina wakati mgumu. Mke wangu ama mkaza mwana, mtu fulani, aniambie ni—nivae tai ya namna gani nayo. Si—sijali kama zinafanana, hata hivyo. Ninataka kupasika kwangu kulingane na Neno la Mungu. Hilo ndilo lipaswalo, maana hapa ndipo mahali ninapokusudia kuishi; si kule chini pembeni pamoja na akina Jones, bali huko ng'ambo Utukufuni aliko Yesu, aliyeenda kutuandalia mahali. Naam, tunataka jambo hilo. Naam, bwana. Epukana na yote haya.

¹⁰⁶ Maskani hii ya dunia hii hapa, unajua ni nini? Mwili huu ni kama koti la kale unalovaa, koti ulilovaa wakati mmoja. Bali sasa una moja ambalo ni zuri zaidi, hulitumii tena. Unafanya nini? Unalining'iniza kwenye kabati ya nguo, kwa kuwa una moja iliyo zuri zaidi. Una koti zuri zaidi. Una koti zuri zaidi. Ni la kisasa zaidi kuliko lile ulilokuwa ukivaa, ambalo limechakaa. Ni nini? Ni lile vazi. Umo ndani ya hilo hapo. Vazi hilo limefanya ninii? Lilichukua umbo lako. Unaona? Bali hulihitaji tena sasa. Umelining'iniza. Ni tambara.

Na hivyo ndivyo huu mwili wa kale ulivyo, wewe, umechukua sura ya ule wa mbinguni. Hata hivyo, si wewe. Wewe umo ndani ya mwili huo. Wewe, Roho wa Mungu, yumo ndani ya mwili huo. Hiyo ndiyo inayoufanya wa nje kutii, kwa kuwa wa ndani unauvuta, unaona, ukiupata na Neno la Mungu; ndani yako, wewe mwenyewe, utu wako.

Mwili huu ni koti la kale tu. Na siku moja, utafanyaje nao, kwa kuwa wewe ulikuwa—ulikuwa katika vazi hilo kwa muda kidogo tu? Huo ni kama vazi la duniani; mwili huu. Ninii wako—mwili wako halisi, utu wako halisi, uko ndani ya koti hili la kale mnaloita William Branham, ama Susie Jones, ye yole yule. Unaona? Siku moja utaning'inia kwenye ukumbi wa kumbukumbu ya duniani kwa ajili yako. Utäuweka huko nje kaburini, na mtu fulani ataweka jiwe la kaburini, "Hapa analala Kasisi *Fulani*, ama Yohana *Fulani*, ama *Fulani*." Utalala pale kama kumbukumbu lako wewe. Watu walikuona tu katika *huu*. Na kile ulichokuwa, wewe halisi, kilikuwa ndani ya huo. Lakini lile koti la kale, lenyewe, "lilichukua mfano wa lile la Mbinguni."

Loo, enyi watu, je! mmeshika nafasi ya kubadilisha makoti? Mmeshika nafasi ya Mbinguni? Kumbukeni, hamna budi kuwa na nafasi zilizowekwa. Hamwezi kuingia bila ya hizo.

Ninawazungumzia katika lugha ya kisasa sasa, mnayoijua. Ukienda hotelini, useme, "Vema, nilikuwa na ninii..."

¹⁰⁷ "Je! ulichukua chumba? Vema, nasikitika. Kila kitu kimejaa." Uko huko nje kwenye baridi, kwa sababu ulishindwa kuchukua chumba.

Na kama ukifikia mwisho wa safari yako ya maisha, bila ya kujiandaa, hakutakuwa na mtu pale kukulaki. Itakulazimu kuingia katika Umilele wenygiza ambako kutakuwa na kupiga mayowe, na kulia, na kuomboleza, na kusaga meno. Huna budi. Huwezi kuuingia ule Mji, wewe, kwa sababu hujaweka nafasi. Huna budi kuweka nafasi, upate kuuingia ule Mji, ambako Yesu ameenda kukuandalia mahali. Kumbuka. Huna budi kujiwekea nafasi, na kuвая vazi la wokovu. Huwezi.

¹⁰⁸ Katika Mathayo, nina Maandiko hapa. Ninaangalia Maandiko, Mathayo, ishirini na... 22:1 hadi 14. Sina wakati wa kuyasoma, kwa kuwa tumechelewa. Nimezungumza kirefu sana, nanyi. Lakini kumbukeni, mfalme alituma na akaandaa chakula cha jioni. Alichinja maksai wake wote, na—na kuwaandaa walio wanono na kila kitu, aliandaa chakula kizuri sana cha jioni. Ndipo akatuma, na akawaalika wengi waje.

Mmoja akasema, "Vema, unajua, hata hivyo, mimi ni mfuasi wa *hili*." "Nami nina jambo *hili*." "Inanipasa kwenda shambani kwangu." Na mmoja akafanya mambo mengi. Ndipo akatuma tena, nao wakawatenda vibaya. Ndipo hatimaye... Hicho kilikuwa ni kizazi cha Wayahudi, ambacho Yesu alikuwa akizungumza nacho. Walikuwa na shughuli nyingine ya kufanya.

Ndipo, hatimaye, akatuma, "Na kusema... Nenda. Usininii tu... Washurutisheni tu. Enendeni mitaani na kwenye barabara kuu, na kila mahali, na mwalazimishe kuingia." Na baada ya jambo hilo, aliyakinia ya kwamba nyumba yake ilikuwa... Karamu yake ya arusi ilikuwa inaenda kuandaliwa. Kutakuwa na wageni mle.

Ndipo akampata mtu mle ndani asiyekuwa amevaa vazi la arusi. Alitaka kushikilia lile koti la zamani. Hebu angalia aliyosema, "Rafiki, baada ya mimi kukualika katika karamu yangu ya arusi, nami nilikualika na kukupa mwaliko wa kuja!"

¹⁰⁹ Na kama ulipata kuwa huko Mashariki, jambo ambalo nililihubiri mara nyingi, karamu hiyo ya arusi ingali inaendelea jinsi vile vile tu ilivyokuwa ikiendeshwa. Bwana Arusi, ambaye, wote, ye ye ana wageni wengi sana ambao atakuwa nao. Labda, Ndugu Kopp, labda umeliangalia jambo hilo kule India. Unaona? Wana wageni wengi sana ambao atawaalika; tuseme atawaalika wageni thelathini.

Sasa, inambidi bwana arusi kutoa mavazi. Inambidi kuyatoa, kwa hiyo kuna mtu anayesimama mlangoni. Nawe unakuja na mwaliko wako. Anachunguza mwaliko wako na

kukuvalisha joho, vazi. Kwamba, baadhi yao ni matajiri, na baadhi yao ni maskini, wengine wao wako vinginevyo, bali wote wanafanana wanapovaa mavazi haya. Wanafanana.

Nanyi nyote mnapaswa kufanana. Hamtakuwa, tuseme, "Mimi *hapa* ni Mmethodisti. *Huku* ni mimi yule Mpresbiteri." Loo, la. Hutaingia, kwanza. Unaona?

Inakubidi kuingia kwa kupitia Mlangoni. Yesu alisema, "Mimi ndimi Mlango wa zizi la kondoo."

"Mimi ni Mpentekoste. Mimi ni wa *hili*. Mimi ni wa *lile*." Hilo halimaanishi chocchote.

Unaingia kwa Mlango ule. Na kama ukija kwa kupitia Mlango ule, unapata vazi.

¹¹⁰ Na mtu huyu, wakati aliposema, "Uliingiaje hapa, rafiki?" Unaona?

Ilionyesha alipitia njia nyingine, na alikuja kupitia dirishani, akaingia kwa njia ya kuhadaa, bali si kwa kupitia mlangoni; si kwa kupitia ule Mlango, jinsi ambavyo Yesu alikuja, kwa kujitoo dhabihu; kumtolea Mungu yote uliyo nayo, na kwenda Kalvari na kusulibishwa pamoja Naye. Na ufufuke tena, upate kuvaavazi Lake la dhabihu na mauti kwa mambo ya dunia.

¹¹¹ "Ukiipenda dunia, ama mambo yaliyo katika dunia, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako." Unaona? Kama ungali una upendo wa dunia, unataka kuenenda kama mlimwengu, na kufanya kama mlimwengu; unajaribu... unaninii... Hata hivyo, wewe uko kanisani, bali ni gugu shambani pamoja na ngano; unapiga makelele pamoja na hao wengine, unafurahi pamoja na hao wengine. Baraka zote za kiroho zikiwa moja kwa moja juu yako.

Unasema, "Vema, nilitoa unabii." Vivyo hivyo na Kayafa naye. Vivyo hivyo na Balaamu. Hilo halina uhusiano wowote...

¹¹² "Nina ubatizo, Roho Mtakatifu." Hilo bado halina uhusiano nalo. Hiyo ni karama tu ya muda kwako.

Karama halisi ni nafsi yako iliyoko kule ndani, unaona, hiyo ilizaliwa na Mungu, na hiyo inatawala jambo lote kwa Neno la Mungu na mapenzi ya Mungu. Na hapo unakua, unaona, ndipo wewe ni mwana na binti ya Mungu. Wewe ni mtoto wa Mungu. Na mambo haya, unapokua... Kama vile mama, sasa wewe uko katika tumbo la ardhi, ukijaribu kutoka. Wewe ni mwana wa Mungu, anayekuja, na unaona Neno likisema, "Inanipasa kufanya jambo *hili*. Ninapaswa kuzaliwa mara ya pili."

"Vema, mimi ni mfuasi wa kanisa." Hilo halimaanishi jambo moja. Unaona?

"Mimi ni Mmethodisti; mama yangu." Hilo lafaa kwa mama yako.

¹¹³ “Vema, jamani, Mimi ni Mpentekoste. Mimi ni mfuasi.” Hilo, kama husimami na hilo Neno, kuna kasoro fulani. Unaona? Ndipo, unaona, baba yako halisi si Mungu. Unaona? Kwa sababu, ule mwanzo halisi nafsi mwako, kabla hata hapajakuwapo na roho, ilikuwa ni nafsi yako. Nafsi hiyo haikutokana na Mungu, basi haikuwa seli zazi ya Mungu, kwanza. Umedanganyika. Wewe ni sehemu ya magugu na unashikilia rekodi ya dunia kwa kutoa magugu. Unatenda kama mlimwengu, ukiipenda dunia, ni kwa sababu kumpenda Mungu hakumo ndani yako.

¹¹⁴ Na sasa kutakuwa na wapakwa mafuta wa uongo katika siku za mwisho, si Yesu wa uongo. Wasingevumilia jambo hilo. Lakini, “wa uongo,” waliopakwa mafuta. Wamepakwa mafuta, naam, bwana, bali wao ni wapinga-Kristo. Wamepakwa mafuta na Roho, kufanya ishara na maajabu ambayo Kristo alifanya, bali hawatalifuata Neno. Unaona?

“Wengi watakuja Kwangu, Siku hiyo, na kusema, ‘Bwana, je! mimi sikutabiri, na kutoa pepo, katika Jina Lako?’”

Yeye atasema, “Ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu. Hata sikuwajua kamwe.”

“Nilikuwa Mpentekoste, Bwana. Utukufu kwa Mungu! Nilipaza sauti. Nilinena kwa lugha. Nami niliweka mikono juu ya wagonjwa, na kuwaponya, nilitoa pepo.”

“Ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu. Sikuwajua kamwe.”

¹¹⁵ Unaona ninalomaanisha? Loo, enyi watoto wadogo, je! mnahisi haja ya vitaminini hiyo usiku wa leo, hicho kitu fulani? Kuna mwili unaongoja huko ng’ambo ya pili. Kuna mwili unaongoja kupokelewa. Enyi watu, msidanganyike. Msidanganyike. Ibilisi ni mdanganyifu. Hata ninii—vazi la arusi, yakubidi ulivae. Halina budi kuvaliwa.

¹¹⁶ Sasa tuko katika wakati wa jioni. Mwili wa duniani sasa uko tayari kuharibiwa, nasi tunajiantaa kuingia katika ule wa Kimbinguni. Na sasa tunasikia mwito wa kigeni, wa Mungu, kwenda katika Edeni hii kuu. Na kabla ya kuzaliwa hapa, miili yetu ya kitoto kichanga lililia kitu fulani ambacho—ambacho kilipaswa kutolewa, la sivo tungekuwa mtoto aliyeteseka hapa kama hatukukipata. Mungu hana mateso kule juu. Wako, kila mmoja wao, amefuata kikamilifu, Bibi-arusi kama tu Bwana Arusi alivyokuwa, Neno lililodhihirishwa katika majira Yake. Mungu, tujalie, usiku wa leo, watoto, kila mmoja wenu! Kuna Mbingu ya kwenda. Kuna kuzimu ya kuepuka.

¹¹⁷ Sasa, wengi wenu mnajua ya kwamba Bwana amenipa maono, maelfu ya hayo. Jambo lililo kubwa kuliko yote... Nilikuwa nikihofu mauti. Yapata miaka mitatu iliopita, Mliona Wafanyabiashara Wakristo, *Ng’ambo ya Pazia la Wakati*. Ninatambua huenda nisimalize usiku huu. Huenda nisiwaone

tena maishani mwangu hapa, bali jambo hili ni kweli. Si—siju kama ningeita hili ono, ama ilikuwa ni kitu gani.

Asubuhi moja, hivi majuzi, nilikuwa... Nilikuwa tu nimeamka. Nilikuwa nimetoka mikutanoni. Na mke wangu alikuwa amelala pale, usingizi. Nikasema, “Kipenzi, uko macho?” Alikuwa akali amelala. Nilijua ilitubidi tuamke, ili kuwapeleka watoto shulenii.

Ndipo nilirudisha mikono yangu nyuma, namna hii, na kusema, “Vema, aisee, Bill Branham, je! unajua umepita umri wa miaka hamsini? Wewe, kama utamfanyia Bwana jambo fulani, afadhali ufanye haraka, maana huna wakati mwinci sana zaidi.” Nikawazia, “Jamani, natumaini ya kwamba ninaweza kuishi kuona Kuja kwa Bwana Yesu.”

Daima nililiwazia, ya kwamba—ya kwamba tulipokufa, ningeona, kwa mfano, ndugu *hapa*. Ningesema... “Naam, ulihubiri kanisani mwangu, usiku mmoja huko duniani, Ndugu Branham.” Lakini, yeze—yeze ni roho, nisingeweza kumpa mkono, kwa maana mkono wake uko huko një kaburimi, umeoza, unaona; wangu, pia. Kwa namna fulani nilikuwa nikiwazia jambo hilo.

¹¹⁸ Lakini asubuhi hiyo, wakati, nilisikia kitu Fulano kikinjia. Nikawazia... Kwa kawaida, kama vile ono linavyokuja. Na nikaangalia, na ni—nikaangalia. Nikawazia, “Jamani! Ni kitu gani hiki?” Nami nikaangalia, vilima vikubwa, vyta kijani kibichi. Na wasichana wakija kutoka katika kila kitu, kwa makumi elfu, na mamia ya maelfu. Nao wote walikuwa wakija, nywele ndefu zikining’nia mgongoni mwao, wamevaa mavazi meupe, miguu mitupu, wakipiga vigelegele, wakishangilia, “Ndugu yetu!”

¹¹⁹ Ni—nikawazia, “Sasa, hili jambo la ajabu.” Niligeuka nyuma na kuangalia. Na mimi huyu pale pale nimelala, na yule pale mke wangu, amelala pale kitandani. Ndipo nikasema, “Sasa, unajua nini? Nilikufa.” Nikasema, “Hivyo, hivyo ndivyo ilivyotendeka. Ni—nimekuifa.” Ndipo nikasema, “Huenda nilishikwa na ugonjwa wa kufa moyo, ama kitu fulani. Nimekuifa. Ule pale mwili wangu umelala.” Nilikuwa tu nimelala pale nimekauka mikono yangu nyuma, namna hiyo, nimekuaka vile vile. Nikawazia, “Ule hauko futi ishirini kutoka kwangu.” Nami huyo pale, nikiangalia. Nikawazia, “Hiyo ni... Yule pale mke wangu. Pale, kile pale kila kitu. Lile pale shati langu limening’nia pale kwenye besera pale. Na kwa hiyo mimi huyu hapa.”

¹²⁰ Nikaangalia kila mahali tena, na wanawake hawa wote walikuwa wakija. Nao walikuwa... Niliangalia, wakiwa wanatokea upande huu, na pale wanakuja ndugu zangu. Loo! Wao ni halisi. Wote walionekana kuwa ni vijana. Walikuwa

wakipiga makelele, “Ndugu yetu mpendwa!” Loo, sikujuu la kuwazia.

¹²¹ Niliwazia, “Ajabu hii.” Nikaangalia nyuma, nami sikuwa mzee. Nilikuwa kijana. Nikawaza, “Hili ni jambo la kushangaza.” Nikawazia, “Je! hili ni ono?” Nikauma kidole changu. Kisha nikawazia, “La. Si kama aina ya ono ambalo nimeona.”

¹²² Ndipo, pale, kitu Fulani kikaanza kuzungumza na mimi *hapa juu*, na kusema, “Umeingia pamoja na watu wako.”

Nikawazia, “Ati pamoja na watu wangu? Je! hawa wote ni Wabranham?”

¹²³ Ikasemi, “Hao ndio waongofu wako uliowaleta kwa Kristo.” Na wanawake hawa . . .

Unajua daima nimehesabiwa, kwa kuwa wameniita “mchukia wanawake,” bali siwachukii. Unaona? Maana, ninaamini . . . Si-si-sipendi wazinzi, wenye tabia mbaya. Ninapenda dada halisi, wa kweli wa Kristo. Kama ndivyo walivyo, sawa.

¹²⁴ Nilikuwa na majeraha nilipokuwa mtoto mdogo. Ninajua mambo yaliyotukia ambayo kwa namna fulani yamegeuza mwelekeo namna hiyo. Lakini hayo—yote yalikuwa ni Mungu, akinininii, akinifinyanga kwa ajili ya wakati huu. Unaona?

¹²⁵ Ninafikiri dada halisi na wa kweli, hakuna kitu kilicho kizuri zaidi. Kama Mungu angempa mwanamume kitu chochote kizuri kuliko wokovu, angempa mke. Unaona? Na kwa hiyo, basi, kama angaliweza kumpa kitu chochote kizuri zaidi, angefanya jambo hilo. Na halafu basi kuona baadhi yao wakigeuka na wala hata hawatendi kama mke, wasio waaminifu kwa nadhiri yao ya ndoa, na waume zao vivyo hivyo. Kumbuka, umefungwa mradi tu ukali hai, mmoja kwa mwinge. “Kile Mungu anachounganisha duniani, kimeunganishwa Mbinguni pia.” Unaona?

¹²⁶ Na kwa hiyo basi ni—niliona jambo hilo. Na wanawake hawa wakakimbia na walikuwa wakinishika, na kunikumbatia, na kuniita, “Ndugu!” Sasa, wao walikuwa ni wanawake, bali hakuwezi kuwa na dhambi mahali hapo. Unaona? Walikuwa ni wanawake. Lakini, unaona, kile kilichotufanya sasa, mwanamke mwenye te—tezi, tezi za kike, na mwanamume mwenye tezi ya kiume, ni kwa ajili ya kuzaa watoto. Haitakuwa kule. Wote watakuwa na tezi moja, bali wangali watakuwa katika umbo lao. Sura ya duniani waliyokuwa nayo hapa itakuwa kule, bali hakutaweza kamwe kuwa na dhambi. Nyote mko sawa. Hakutakuwa na watoto tena watakaozaliwa kule. Unaona? Hiyo ni kweli. Yote itakuwa hivyo. Na hivyo basi mimi nikaangalia, na hawa wanawake.

¹²⁷ Ndipo wakanichukua juu. Hawa ndugu wakaniweka mahali fulani. Nikasema, "Kwa nini mnafanya hivi?"

Yeye akasema, "Duniani ulikuwa kiongozi." Kisha akasema—kisha akasema, "Wewe... Hawa ndio wale watu."

¹²⁸ Na kulikuwa na mwanamke fulani aliyejitokeza. Kasema, "Ndugu yetu wa thamani." Mwanamke mzuri sana!

Alipopita pale, Sauti hii ikanyamaza, ikasema, "Humkumbuki?"

Nikasema, "La."

Kasema, "Ulimwongoza kwa Kristo wakati alipokuwa amepita umri wa miaka tisini. Unaona? Hivi huwezi kuona ni kwa nini anasema 'ndugu wa thamani'?"

Nikasema, "Vema, u—unaenda..."

Kasema, "La. Tunangoja hapa."

Nikasema, "Vema, kama nimeaga dunia, ninataka kumwona Yesu."

Kasema, "Huwezi kumwona sasa. Haya ni Maandiko, yalisema, 'Roho zilizokwu chini ya madhabahu.' Yeye yuko juu kidogo tu. Siku moja Yeye atarudi. Tutarudi duniani. Hatuli wala hatunywi hapa."

¹²⁹ Nikasema, "Unataka kusema nilikuwa na hofujuu ya jambo hili? Mbona, hii..."

Hakuna neno la kusema jambo hilo, enyi marafiki. "Ni pakamilifu," lisingepagusa, "adhimu." Hakuna msamiati wa Kiingereza ninaojua, hakuna neno kamwe, lingaliweza kuelezea jinsi palivyo. Ni zaidi ya kitu chochote ninachoju. Huyo hapo. Hakukuwa na magonjwa, hakuna huzuni. Usingeweza kufa. Usingeweza kutenda dhambi. Palikuwa ni pakamilifu kabisa, pakamilifu kabisa. Enyi marafiki, haiwapasi, haiwapasi kupakosa. Kumbukeni.

¹³⁰ Na nilipokuwa mvulana mdogo, niliona ono la kuzimu, kama mvulana mdogo. Nanyi mnajua jinsi ambavyo mabibi, siku hizi, ama wanawake (mabibi wasingeefanya jambo kama hilo), wanavyojipaka rangi macho yao kama mbwa mwitu, ama kitu kama hicho, kitu kile cha bluu chini ya jicho lao. Niliona jambo hilo. Nilikuwa nikizama. Kama mvulana mdogo, nilikuwa nimepigwa risasi, nami nilikuwa nimelala, nikifa hospitalini. Nami daima nilikuwa nikijua kulikuwa na Mungu.

Ninakumbuka maombi ya kwanza nililowahi kujaribu kuomba. Jambo pekee ningaliweza kusema... Si—sijasimulia jambo hili hapo awali. Ninajisikia tu nilisimulie sasa hivi. Nilikuwa nimepigwa risasi, nimelala pale, nikifa huko kondeni. Na ombi pekee ningaliweza kuwa nalo kwa Mungu, nilisema, "Unajua, Bwana, mimi kamwe sijapata kufanya uzinzi." Unaona? Kama maskini mvulana mdogo yapata umri wa miaka

kumi na mitano, nilijaribu kuishi msafi. Ndipo nikasema, “Nimeishi msafi.” Na hilo tu ndilo ningaliweza kusema. Hayo ndiyo matendo mema pekee niliweza kumpa Yeye.

¹³¹ Na ndipo nimelala pale, basi, wakati daktari walipoondoka pale nilipo, na nikajisikia nikizama katika Umilele wenygiza, ilivyoonekana. Nilimlilia baba, “Ee, baba, nisaide.” Hakukuwa na baba kule. “Mama, nisaide.” Hakukuwa na mama kule. “Mungu, nisaide.” Hakukuwa na Mungu kule. Ilikuwa ni jinamizi tu lisilo na mwisho, lenye kuchukiza. Kuzimu kunakowaka moto mkubwa kungekuwa ni raha, ukiwa juu kando yake. Na wakati nikiangukia kule, nikawaza, “Loo, jamani!” Kufingirika na kufingirika, namna hii. Nilifikia mahali, moshi, na giza, na maradhi. Na, loo, kujisikia kwa namna hiyo! Ilikuwa ni mauti kwangu.

Ningeweza kuwaona hao wanawake wakija kwangu, wakiwa na hayo macho yaliyopakwa rangi namna hiyo. Sasa kumbukeni, hilo limekuwa ni miaka arobaini na mitano, yapata miaka arobaini iliopita, hata hivyo. Wakifanya, walikuwa wakifanya, “Oooh! Oooh! Oooh!”

Nikasema, “Hivi nitakuwa kule milele?”

“Milele.”

¹³² Nikasema, “Ee Mungu, kama utanitoa humu, kamwe si—si—sitakuonea aibu tena. Sitakuonea aibu kamwe. Mungu, naomba unipe kujaribu tena.”

Muda si muda, niljisikia nikirudi. Naye daktari alipigwa na bumbuwazi, maana moyo wangu ulikuwa ukipiga tu mara kumi na saba kwa dakika. Nilikuwa tayari nimetokwa na damu yangu yote na kila kitu, nilikuwa nimelala katika damu yangu mwenyewe. Nami nimeshangaa, hivi siku moja jambo hilo litatukia?

¹³³ Yapata miaka miwili iliopita, nilipohamia Tucson, nilikuwa na mke wangu kwenye duka kubwa la J.C. Penney. Nilikuwa nimeketi kule namna *hiyo*, huku nimeinamisha kichwa changu, nikingojea. Maana, mnajua jinsi ambavyo, akina mama, wanazunguka dukani kwa muda mrefu. Nami nilikuwa—nilikuwa nimeketi pale, nimeinamishwa kichwa changu kimeinamishwa chini namna *hii*. Na lift ilikuwa ikipanda. Na hawa hapa baadhi ya hao wanawake wanakuja, wakiwa na mtindo wa kukata nywele kichwa maji, mwajua, kama wanavyofanya, namna *hiyo*. Wakija na hayo macho yaliyooonekana yamepakwa rangi namna hiyo. Nao walikuwa wakizungumza Kihispaniola. Na jambo ndilo hilo. Lote (lile ono) lilitukia tena. Hilo hapo, “Oooh! Oooh!”

¹³⁴ Ndugu, dada, hebu niwaambie jambo fulani. Linaweza kuonekana ni la kuchekesha hivi sasa, bali hebu ufile kule mara moja. Ni jambo zito. Kamwe usiiedee njia hiyo.

¹³⁵ Mimi, kama mzee, mhudumu, nimehubiri kote duniani, nina mamilioni ya marafiki, bali ninajua sina budi kusimama na ninyi huko ng'ambo. Yakimbieni mambo ya ulimwengu. Na kama kuna kitu fulani ndani yako, kwamba ungali unataka kutenda jinsi unavyotenda, kama una mambo ya ulimwengu ndani yako, kumbuka, wewe si wa Mungu. Wewe ni mfuasi tu wa kanisa, mpaka wito huo; kile kilindi, kikiita Kilindi. Unaona?

¹³⁶ Kama vile, kabla hapajakuwa na pezi juu ya mgongo wa samaki, ilibidi kuwepo na maji apate kuogelea, kwanza, la sivyo asingekuwa na pezi kamwe.

Kabla hapajakuwapo na m—mti wa kuota duniani, ilibidi pawe na ardhi, la sivyo kusingekuwako na mti wa kukua ndani yake. Kusingekuwa na sababu yo yote kwa huo mti kuwapo, na kuufanya uwe pamoja nayo.

¹³⁷ Kabla hapajakuwa na uumbaji, hapana budi pawe na Muumba. “Heri wenye njaa na kiu ya haki.” Unaona? Kuna kitu fulani ndani yetu. Uliinua mkono wako muda mfupi uliopita, “Ninamhitaji Mungu zaidi.” Unaona? Kuna kitu fulani kinachohitajika.

Na kama unaupenda ulimwengu, ukiienda njia hiyo, mambo ya ulimwengu, utaiienda njia ya ulimwengu, nawe utaanguka. Unaona? Tokeni. Ninyi ni wana na binti za Mfalme, yule Mfalme. Iweni bibi na wangwana. Enendeni kama Wakristo. Ishini kama Wakristo. Mwe na tabia kama Wakristo. Kumbukeni, nitakutana nanyi kwenye Kiti cha Hukumu pamoja na matamshi haya. Unaona?

¹³⁸ Angalia katika kioo chako cha kuangalilia, usiku wa leo, na uone. “Ninalekea wapi? Je! Yesu ananiandalia mahali, mwili? Mwili huo ni mkamilifu. Mwili huo unaenda kwa uangalifu. Ni mwana ama binti mbele za Mungu. Nami *hapa* niko katika utungu wa kuzaa, kuzaliwa katika mwili ule pale. Kama ningali ninaupenda ulimwengu, inaonyesha ya kwamba (mimi si) sina mwili kule. Mimi ni mfuasi tu wa kanisa. Sikuwa seli zazi ya Mungu. Mimi si seli zazi. Yeye si Baba yangu.”

¹³⁹ Yeye alisema, “Msipostahimili marudio,” hayo ndiyo mnayoyapata sasa, “basi ninyi ni watoto haramu, wala si watoto wa Mungu.” Hiyo si ni kweli [Kusanyiko linasema, “Kweli.” —Mh.] Je! si Biblia inasema jambo hilo? “[Amina.]”

Kama huwezi kustahimili marudio ya Mungu, unapoona Maandiko yakikuweka sawa, nawe unasema, “Loo, sitaki kusikia Upuuzi huo. Mi—mimi ni Mkristo. Ninafanya ninii...” Vema. Endelea. Unaona? Hilo ni thihirisho moja la hakika ya kwamba wewe si mwana wa Mungu.

Bali mwana halisi wa Mungu anaona njaa na kiu. Kwa nini? Kama kuna jambo fulani moyoni mwako, kikikwambia unataka jambo hilo, na linahitajika humo, inaonyesha kuna kitu fulani kinachodundadunda, kikijaribu kukuvuta kule. Kuna mwili

fulani kule, ambao *huu* hapa ni mfano wake. Unautumia huu kwa ajili gani, kumtukuza Ībilisi na ulimwengu, na mitindo na kadhalika? je! unaelekeza uso wako Mbinguni, kuna kitu fulani kule, je! unamtkuza Mungu kwa maisha yako?

Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia. Nami ninaenda kuwaandalia mahali.

. . . nitakuja tena, kuwakaaribisha kwangu; ili nilipo mimi, nanyi mwepo.

¹⁴⁰ *Mambo Yatakayokuwapo.* Mambo haya yaliyopo sasa, ni uwezekano tu, yakiita mambo yatakayokuja.

Na tuombe.

¹⁴¹ Wazieni kwa uzito sana. Je! mtafanya hivyo, enyi wapenzi marafiki Wakristo? Wazieni jambo hilo kwa uzito sana, kwa muda mfupi. Hebu na tunyamaze sana kwa muda kidogo. Hebu Roho Mtakatifu azungumze.

Sasa, Bwana Yesu alinituma kwenu Wapentekoste, muda mrefu uliopita. Huyu hapa mmoja wa wavulana wenu ambaye amekuja kuwa mchungaji wenu, kasema, “Ilitokana na huduma hii.” Yeye alimwona Bwana Yesu akiyafungua macho ya vifofu; “kufanya,” yeye alisema, “vichwa maji kukoma mara moja.” Ningali nina ibada za uponyaji. Lakini ninatambua ya kwamba nimewaombea watu wengi waliokuwa wagonjwa sana. Waliponywa. Bwana aliyajibu maombi, na kuwaponya wagonjwa. Lakini, unajua, baadhi ya watu hao, walioponywa, tayari wamekuifa. Na haidhuru wewe ni mgonjwa jinsi gani, kama ukiponywa, utakufa, haidhuru.

Lakini hiyo nafsi, ndugu yangu wa thamani, nafsi hiyo, dada yangu wa thamani, je! hutawazia jambo hilo sasa? Hiyo ni ya Milele. Kama upendo huo wa Mungu hauko humo ndani, hakuna kitu kinachovuta, hivi hutamwuliza Mungu, “Ee Mungu, nianzishe tena, upya, usiku wa leo. Ninakupenda, Bwana. Ninataka kukupenda. Na kitu fulani moyoni mwangu kinaniambia ya kwamba inanipasa kuambatana karibu na Wewe. Ninataka kuja, sasa hivi, Bwana, na kufanya jambo hilo”? Kama mtu huyo ama watu hao wamo katika jengo hili ama nje ya jengo hili, ninawasihi, kama mtumishi wa Kristo, katika Jina la Yesu Kristo, je! mtaninii tu, huku vichwa vyenu vimeinamishwa, umwinulie Mungu mkono wako na kusema hivi, “Mungu, nivute karibu, karibu, Mungu mpenzi. Ninataka kukubaliana na kila kitu ulicho nacho katika Neno Lako”? Inueni mikono yenu. Sasa iweni waaminifu sana. Wazieni tu.

¹⁴² Sasa, wao wanasema, “Loo, nimefanya jambo hili. Nime-, nimepaza sauti kwa nguvu, Roho. Nimesema kwa lugha. Lakini, angalia, kuna kitu fulani kinachokosekana maishani mwangu. Ninaangalia katika koo cha Neno la Mungu, ninajua kuna kitu

fulani. Ninaenda kanisani, bali mimi siko vile ninavyopaswa kuwa.” Unaona? Hilo inaonyesha, jambo fulani.

Sasa, kama unaweza kujiangalia mwenyewe na kuona kwamba hukubaliana na Neno la Mungu, na hakuna kitu ndani humo kitakachokufanya uinue mkono wako, basi unajua kuna kasoro fulani. Una kasoro. Kuna... Mama alizoea kusema, “Huwezi kupata damu kutoka kwa tanipu, kwa kuwa hamna damu ndani yake.” Unaona? Wazia jambo hilo, kwa uzito sana. Hii huenda ikawa ndiyo nafasi yako ya mwisho. Mikono thelathini, arobaini imeinuliwa, kundi hili ndogo hapa, hata ya makasisi.

¹⁴³ Iweni na uchaji kabisa kwa muda kidogo tu. Sasa wazieni kwa makini sana. “Mungu mpenzi, huenda nikauawa, usiku wa leo, katika ajali. Huenda nikafa kwa ugonjwa wa moyo. Moja ya asubuhi hizi, huenda nikamwita daktari, naye aje, na pigo langu la moyo linapiga kwenye mkono wangu wa shati; nimeaga dunia. Ninagandamiza shavu langu kwenye mito, nikiita, ‘Ee Mungu! Ee Mungu! Ee Mungu!’” Unaona? Moyo huo unapiga pigo lake la mwisho. Unakaribia kwenye ule Mlango mkubwa. Kamwe hutatoka isipokuwa umezaliwa mara ya pili na Roho wa Mungu. Kamwe hutatoka isipokuwa kuwe na kitu fulani ndani yako, ukiisha kuzaliwa na Roho wa Mungu, ukiona njaa na kiu ya kuendelea pamoja na Mungu. Haina budi kuwa. Unaona? Wewe ni mtoto duniani, katika tumbo la ardhi, bado ukingojea kuzaliwa katika Ufalme wa Mungu, ambako ameenda kutayarisha mwili mwingine kwa ajili yako, ambao ni mwili mkamilifu.

Sasa wazieni kwa kina kabisa, na hebu tuombe pamoja.

¹⁴⁴ Mungu mpenzi, kwa kuwa ninajua ya kwamba haya yamewekwa kwenye kurasa za Kitabu, ile kumbukumbu kuu! Tumekosea katika sayansi, Bwana, vya kutosha kutuamsha, kwenye kweli kujua kwamba kila hatua tunayochukua inazunguka na kuzunguka kote ulimwenguni, wakati huo huo tunaposogea. Tumejua hayo kupitia katika televisheni. Tunatambua, Baba, ya kwamba hiyo televisheni haitengenezi picha, inaelekeza tu mi-mitetemeko hiyo kwenye chubu inayotengeneza picha? Hata rangi ya nguo tunazovaa, zinaonyesha kupitia kwenye mawimbi ya etha yaliyoko juu ya hewa, mitetemeko hiyo kote ulimwenguni. Basi vipi dada zetu waliovaa nguo hizo, wanaotenda hivyo, wala hata hawana njaa; wamejipaka rangi nyusoni, wakakata nywele?

Wahudumu ambao wangeenda kwenye theolojia, seminari fulani, “Na kuamini neno la mwanadamu, ambaye anafanya, kwa mapokeo yao, wanazitangua amri za Mungu kwa watu, kwa mapokeo yao,” wakisema wanapaswa kuwa wafuasi wa kanisa, na ni hivyo tu?

Ee Mungu, hivi wao wanatambua ya kwamba kila neno tunalosema, imethibitishwa kisayansi, liko kwenye kumbukumbu? Na inaanza tunapoanza kuishi katika ulimwengu huu. Inaisha tunapokufa, na inawekwa kwenye albamu ya Mungu, ipate kuchezwa tena kwenye ile Hukumu.

Tutaepukaje jambo hilo, hukumu ya Mungu, kama jambo hilo limefanywa dhahiri sana mbele zetu na hata hivyo tunalikataa?

Ee Mungu mpenzi, maneno haya hayafi kamwe. Yanaendelea na kuendelea. Kumbukumbu itachezwa kwenye Siku ya Hukumu. Uliona mikono hiyo ilioinuliwa, Baba. Itakuwa papo hapo kwenye Siku ya Hukumu. Pia, jinsi mioyo yao ilivyokuwa ikiwazia, itakuwa pale kwenye Siku ya Hukumu.

¹⁴⁵ Sasa, Baba, Mungu, ninakuomba, kama mtumishi Wako, ninaomba ya kwamba utaondoa uovu wote kutoka kwa watu Wako. *Uovu:* jambo ambalo tunajua tunapaswa kulifanya, wala hatulifanyi. Daudi alisema, “Kama nikiwazia uovu moyoni mwangu, Mungu hatayajibu maombi yangu.” Ninaomba, Mungu, ya kwamba utachukua uovu wetu, maana Neno ndilo kioo Chako cha kujiangalia kinachotuonyesha jinsi tulivyopungukiwa kuwa wana na binti za Mfalme. Baba, ninaomba ya kwamba utafanya jambo hilo, usiku wa leo.

¹⁴⁶ Na ufanye hiyo kuwa madhabahu, maana madhabahu yamejaa watu. Na ufanye hiyo kuwa madhabahu, hapo kwenye kititambalo wameketi, ufanye huo moyo wao kuwa madhabahu. Jalia ulimwengu uondoke kutoka kwa kila ndugu, dada hapa ndani. Na jalia ile seli zazi ya Uzima, jeni ya Mungu ambayo tumezungumza tu kuihusu, ile sifa iliyotoka kutoka kwa Mungu, na imedhihirishwa hapa kumheshimu na kumtukuza Mungu. Mungu, uondoe ulimwengu kutoka huko.

¹⁴⁷ Hao wengine, siwezi kuomba, Bwana, kwa sababu, “ugonjwa ni wa mauti,” wala hukuna kitu pale kinachowafanya kusogea. Lakini wale wanaoweza kusogea, na wanajua ya kwamba ni kosa, isafishe mioyo yao na nafsi zao, usiku wa leo, Baba. Na jalia wajazwe na Roho Wako, watembee katika Nuru Yako.

¹⁴⁸ Mbariki maskini mpenzi mchungaji huyu kijana, mwenye afya, anayeonekana ni mwenye nguvu hapa, Bwana. Mvulana huyu, alishawishika, alisema, kwa yale aliyokuona Wewe ukifanya. Mvulana huyu mzuri, Ee Mungu, iwashe moto nafsi yake. Tujalie, Bwana. Jalia awe mchungaji wa kweli, bila kukoma, wakati wote, apate kulilisha kundi ambalo Roho Mtakatifu amemfanya msimamizi juu yake. Tujalie, Bwana. Jalia asigeuke mkono wa kulia ama wa kushoto, kamwe kwa kanuni yoyote ya imani, wala chochote kile bali Neno lisiloghoshiwa la Mungu likitoka kinywani mwake, na Hilo peke yake. Mbariki, Mungu, ye ye na wapenzi wake, na maskini kanisa lake hapa. Kuwa pamoja nao wote, Baba.

¹⁴⁹ Ninakabidhi haya Kwako, Baba. Mbegu imepandwa tayari. Jalia iangukie mbegu ile iliyochaguliwa kwa ajili ya Uzima, na kukua wawe Wakristo wakuu, na wenye nguvu kwa ajili ya kusanyiko hili hapa, na makusanyiko mengine ambako wanatoka. Tujalie, Bwana. Ninayakabidhi Kwako, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu.

Na, Baba, “Alijeruhiwa kwa makosa yetu, akachubuliwa kwa uovu wetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake; na kwa wake sisi tumeponywa.”

¹⁵⁰ Nilimwona maskini mwanamke mwenye wasiwasi, muda mfupi uliopita, akipitia mlangoni. Na, Ee Mungu, katika familia yake, ni mambo makuu jinsi gani yaliyofanywa, jinsi ambavyo umejidhihirisha! Ninaomba, Mungu, kwa ajili ya mwanamke huyo. Ondo hayo yote ya nyuma, maisha, Bwana, na umponye usiku wa leo. Utafanya hivyo, Bwana? Mchukue Kwako.

¹⁵¹ Unaona jambo hilo, watoto wadogo wakiketi hapa, Bwana, wakihitaji uponyaji, wengine. Ninaomba ya kwamba utawaponya, Baba. Tujalie. Jalia nguvu Zako kuu za uponyaji zije na zikatuponye, nafsi na mwili pia.

¹⁵² Na sasa, kwenu ninyi mliono kanisani hapa, ama huko nje mnaohitaji uponyaji, ninataka mwinue mkono wenu, mseme, “Ninahitaji uponyaji, Ndugu Branham.” Inaonekana kana kwamba kila mtu anahitaji. Vema. Je! mtaniamini mimi kwamba ni mtumishi wa Kristo? Semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Basi, ninataka mweke mikono yenu mmoja juu ya mwingine. Hebu wekeaneni tu mikono. Ninyi mlionua mikono yenu, mliono ndani ama nje, inueni mikono yenu, kwamba ninyi mlikuwa ni waamini katika Mungu.

Yesu Kristo alisema, agizo Lake la mwisho kwa Kanisa, “Enendeni ulimwenguni mwote, na mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Yeye aaminie... Yeye aaminie na kubatizwa ataokoka. Asiyeamini atahukumiwa. Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; katika Jina Langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; wakashika nyoka ama kunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru; tena, wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Sasa, Yesu alisema hayo. Kumbukeni, Yeye alisema hayo. Hayo hayana budi kutimia. Asingelisema hilo pasingekuwapo na mtu atakayelishika Neno hilo.

Kama tu vile tumbo la uzazi la Mariamu lingeweza kushika seli zazi, “Bikira atachukua mimba.” Kama vile mtende ungeweza kuumbwa, mwaloni juu ya kilima, Neno Lake lilifanya jambo hilo.

Neno Lake linaweza kuingia moyoni mwako sasa hivi. “Mimi ni mwamini, Bwana. Mwanamume huyu ama mwanamke niliyemwekea mikono, wanateseka. Sijombei mwenyewe. Kwa sababu, wao wananiombea. Ninamwombea mwanamke huyu, ama mwanamume huyu. Na, Ee Mungu, mponye mwanamume

huyu, ama mwanamke huyu. Nami ni mwamini, na sasa tumekusanyika. Tumefundishwa tu ya kwamba tulikuwa pamoja na Kristo hapo alipotembea duniani, kwa kuwa sisi ni sehemu ya Neno Lake. Tuliteseka pamoja Naye. Tulimwaga damu pamoja Naye. Tulikufa pamoja Naye. Tulizikwa pamoja Naye. Tumefufuka pamoja Naye, nasi tumekeeti pamoja katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu. Yule Mfalme mkuu akiketi hapa mionganoni mwetu, nami ni mwana ama binti wa Mfalme huyu. Nami nimeweka mkono wangu juu ya mwana ama binti wa Mfalme, ambaye ananiombea, nami ninawaombea. Sasa, Bwana, jibu ombi langu, na umponye huyu mwana wa Mungu ama binti ya Mungu.”

Pamoja, hebu na tuombeane sasa sisi kwa sisi.

¹⁵³ Bwana Yesu, tunakuja kwa unyenyekevu, tukikiri makosa yetu. Tunakuja, tukikiri ya kwamba sisi tunastahili magonjwa na mauti, na huzuni, bali tunakubali upatanisho Wako kwa ajili ya dhambi zetu na maradhi. Na, usiku wa leo, wana hawa na binti za Mungu, wanaoketi hapa, wanasiliza sahihisho la Neno, na wanainua mikono yao, na wanataka kuwa karibu zaidi. Wanawekeana mikono wao kwa wao sasa kwa sababu wanaamini Neno Lako kuwa ni kweli. Wanaamini sasa kwamba tumefufuka pamoja na Kristo, tumekeeti katika ulimwengu wa Roho pamoja Naye. Wamewekeana mikono wao kwa wao, wakiombeana.

Ulisema, “Maombi ya imani yatawaokoa mganjwa, Naye Mungu atampa afya; na kama amefanya dhambi yoyote, itasamehewa kwake. Mkiungamaniana makosa yenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa. Kwa kuwa maombi ya bidii ya mwenye haki yana nguvu nyingi.” Ee Mungu wa Milele, yasikie maombi ya watumishi Wako.

Na sasa, imeandikwa tena, “Kama watu, walioitwa kwa Jina Langu, watakusanyika pamoja, na kuomba; basi nitasikia kutoka Mbinguni.” Ee Mungu, yasikie maombi ya watoto Wako usiku wa leo, kutoka Mbinguni. Mtume Roho Mtakatifu juu ya wasikilizaji hawa, kama upepo wa nguvu ukienda kasi. Nasi tunawaleta watu hawa mbele za Mungu.

¹⁵⁴ Shetani, umeshindwa. Wewe ni kiumbe kilichoshindwa. Yesu Kristo alikushinda huko Kalvari. Huna nguvu. Wewe ni mdanganyifu. Tunakupa changamoto, usiku wa leo. Katika Jina la Yesu Kristo, watoke watu hawa hapa, enyi maradhi na magonjwa. Na waende, wakiwa huru, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu.

¹⁵⁵ Haleluya! Mnahisi utukufu wa Mungu! Mnahisi maombi yako yakijibiwa. Unaamini Mungu alimjibu mtu anayeketi karibu nawe? Ni wangapi wanaoamini jambo hilo? Inueni mikono yenu. [Kusanyiko linafurahi—Mh.] Haya basi. Loo, ajabu!

Ninampenda, Ni- . . .

Huku mikono yenu imeinuliwa juu sasa, mwimbieni, kwa moyo wenu wote.

Kwani kwanza alipenda . . .

Je! unamaanisha jambo hilo, kwa moyo wako wote sasa?

¹⁵⁶ Ni wangapi wenu wanajisikia ya kwamba Mungu amesamehe maovu yenu, mambo ambayo mmefanya? “Na tangu usiku huu na kuendelea, Ee Mwana-Kondoo wa Mungu, ninaahidi kutembea kwa uadilifu. Nitatembea kwa heshima ya Jina ambalo nimeitwa, Mkristo, maisha kama ya Kristo. Nitainua mikono yangu, Mungu. Ninajiweka wakfu upya Kwako, usiku huu. Nitatembea katika Nuru.” Amina.

Tutatembea Nuruni, Nuru nzuri,
 Inakuja toka ambako matone ya umande
 yanang’aa;
 Angaza kote kutuzunguka, mchana na usiku,
 Yesu, Nuru ya ulimwengu.
 Tutatembea Nuruni, Ni nuru nzuri sana,
 Inakuja toka ambako matone . . .

Ambako ameenda kutuandalia mahali.

Angaza kote kutuzunguka, mchana na usiku,
 Yesu, Nuru ya ulimwengu.
 Njoni, enyi watakatifu wote wa Nuru
 mkatangaze,
 Yesu, Nuru ya ulimwengu;
 Ukweli na rehema katika Jina Lake,
 Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Tutafanya nini basi?

Tutatembea Nuruni, Ni nuru nzuri sana,
 Inakuja toka ambako matone ya umande
 yanang’aa
 Angaza kote kutuzunguka, mchana na usiku,
 Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Loo, hivi husikii umesuguliwa kabisa, unajisikia vizuri?
 [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Loo, jamani! Hebu tupeane mikono, tunapoimba tena.

Tutatembea Nuruni, Ni Nuru nzuri sana,
 Inakuja ambako . . . (Mungu akubariki,
 ndugu.) . . . ya rehema yanang’aa;
 Angaza kote kutuzunguka, mchana na usiku,
 Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Hebu tufunge tu macho yetu na kuuvumisha. [Ndugu Branham na kusanyiko wanaanza kuvumisha Yesu, *Nuru ya Ulimwengu*—Mh.] Tutatenda kama watoto. Sisi ni watoto.

Lo, ni Nuru nzuri sana,
 Na inakuja ambako matone ya umande
 yanang'ara;
 Loo, angaza kote kutuzunguka, mchana na
 usiku,
 Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Hivi hamumpendi Yeye? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—
 Mh.]

Yesu kwa imani,
 Nakutumaini, . . .

Hebu fungeni tu macho yenu na muuimbe. Abuduni
 katika Roho.

Peke Yako;
 Nisikie sasa
 Na kunitakasa
 Ni wako kabisa
 Tangu leo!
 Nipe nguvu pia
 Za kusaidia
 Moyo wangu;
 Palipo na giza,
 Utaniongoza,
 Hivi nitaweza
 Kufuata.

¹⁵⁷ Loo, jamani! Ninajua mimi ni jamaa tu wa mtindo wa kale.
 Ninapenda . . . Nafikiri hiyo imeshinda maigo haya yote mapya
 yaliyokatwa-katwa, ya dansi za roki, maili milioni moja. Hao
 washairi wa kale, walioandika hizo nyimbo, Roho Mtakatifu
 aligusa kalamu hiyo, wakaanza kuandika. Loo, jamani! Wazieni
 juu Eddie Perronet na hao wote; watu mashuhuri! Fanny Crosby:

Usinipite Mwokozi,
 Unisikie.

¹⁵⁸ Wakati mmoja walikuwa wakijaribu kumpata. Hakufanya—
 hakufanya kama Mpentekoste Elvis Presley, kuuza haki yake
 ya mzaliwa wa kwanza kwa ajili ya lundo la Makadilaki.
 Yeye . . . Walimjia na kumtaka awatungie—awatungie nyimbo za
 kilimwengu. Akasema, “Nisingefanya jambo hilo, hata kidogo.”

Kasema, “Mbona, wewe ni kipofu. Utakapofika Mbinguni,
 utajuaje?”

Akageuka, uvuvio, kwa hiyo akasema:

Nitamjua, nitamjua,
 Na nitasimama karibu Nayé nikiisha
 kukombolewa;
 Nitamjua, nitamjua (Vipi?)
 Kwa alama za misumari kwenye ninii Yake . . .

Vinginevyo, "Nisipomwona, nitaupapasa mkono Wake."

Nitamjua, nitamjua,
Na nitasimama karibu Naye nikiisha
kukombolewa;
Nitamjua, nitamjua
Kwa alama za misumari mkononi Mwake . . .

¹⁵⁹ Hivi hiyo haiwafanyi kumpenda? Ameenda kutuandalia mahali! "Na nikienda kuwaandalia mahali, nitarudi tena, kuwapokea Kwangu."

¹⁶⁰ Enyi watoto wadogo mlio katika uchungu sasa, tiini tena amri za Mungu. Na mchungaji, hapa, kama hakuna hata mmoja wenu aliyekwisha kubatizwa, maji yatakuwa tayari. Na—na ufuasi wa kanisa, ama lolote mnalotaka kufanya ama lolote lile, fanyeni. Kama huna ubatizo, Roho Mtakatifu, huu ndio usiku wa kumpokea. Hivi hamwamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

¹⁶¹ "Loo," unasema, "Ndugu Branham, tumechelewa. Umehubiri kwa muda mrefu."

Paulo alihubiri usiku kucha, usiku mmoja, Ujumbe wa aina hii. Na ninii mdogo... Kijana mwanamume akaanguka kutoka ukutani na kujiu. Naye Paulo, akiwa amepakwa mafuta sana na Ujumbe wa namna hiyo, aliweka mwili wake juu yake, ndipo uhai ukamrudia tena. Yeye ngali "Yesu Kristo ye ye yule jana, leo na hata milele."

Hivi hamumpendi Yeye? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hebu tuninii tu, mara nyingine tena, huku mikono yetu imeinuliwa, "Ninampenda. Ninampenda."

Yuko wapi mwenye kupiga piano? Pale, tafadhali, dada, ye yote yule. Tupe sauti yake, tafadhali.

Ni wangapi wanaompenda? Hebu inua tu mkono wako. Useme, "Kweli ninampenda. Ninampenda tu, kwa—kwa moyo wangu wote. Ninampenda."

¹⁶² Sasa hebu na tuuimbe, kwa utukufu wa Mungu. Sasa, huku macho yetu yakiwa yamefumbwa, mikono yetu imeinuliwa Mbinguni, "Nampenda. Nampenda." Tutamwabudu. Unapohubiri, na kukata, na kurarua, na kuvuta namna hiyo, hii ndiyo zeri ambayo Mungu anamwaga, inap onya tu. "Kuna zeri huko Gileadi, kwa ajili ya nafsi." Hebu tuimbe sasa. Tupe sauti.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

¹⁶³ "Na katika jambo hili watu wote watajua ya kwamba ninyi ni wanafunzi Wangu, mnapopendana, mmoja kwa mwingine."

Hiyo ni kweli. Kama hatuwezi kupendana wale tunaowaona, tutampendaje Mungu Ambaye hatuwezi kumwona?

Nampenda.

¹⁶⁴ [Ndugu Branham anazungumza na ndugu fulani jukwaani—Mh.] Mungu awabariki. [Ndugu huyo anasema, “Kuwa hapa usiku wa leo ni heshima halisi kutoka Mbinguni.”] Asante, ndugu. [“Kweli inapendeza.”] Sasa, nafikiri kanisa, kila mmoja, alitiwa nguvu. Nanyi je? [“Naam. Kweli.”] Mungu akubariki, Ndugu Boone. Nitalirudisha kusanyiko kwako. Mungu akubariki.



MAMBO YATAKAYOKUWAPO SWA65-1205
(Things That Are To Be)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ultolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, tarehe 5 Desemba, 1965, katika First Assembly Of God kule Rialto, California, Marekani, umetolewa kwenvye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings.

SWAHILI

©2008 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org